

**Mabirika Yavujayo**  
Jeffersonville, Indiana, USA  
Julai 26, 1964J

1 Hebu na tuombe. Bwana, sasa tunaamini. Tunamwamini Mwana wa Mungu, na, kupitia jambo hili, tunakubali Uzima wa Milele kupitia Kwake. Sasa tumekusanyika tena, alasiri ya leo, ama jioni hii, kwa ajili ya ibada nyingine, tukikutumainia Wewe kwa ajili ya Ujumbe na yale utakayotuambia usiku wa leo. Tunakuamini Wewe, Bwana, na tunakungojea. Nawe ulisema, "Hao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya; watapaa juu kwa mabawa kama tai." Nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba utatupa hizo Nguvu za kupaa juu, usiku wa leo, tunapokungojea Wewe.

Tunakushukuru kwa ajili ya watu hawa, na kwa yale wanayomaanisha Kwako na yale wanayomaanisha kwangu. Ninakushukuru kwa ajili ya jambo hilo, Baba. Wao ni vito Vyako. Nami ninaomba, Mungu, ya kwamba usiku wa leo, ya kwamba utajidhihirisha Mwenyewe njiani, kwao, kwamba wana hitaji. Kama kuna wagonjwa hapa, jalia waponywe. Kama kuna shaka katika nia ya mtu fulani; iondoe, Bwana. Na utupe tu Uwepo Wako na baraka Zako, kwa sababu tunazihitaji, Bwana. Wewe ndiwe utoshelevu wetu wote. Na, bila Wewe, hatuwezi kufanya lolote.

Tunaomba ya kwamba utapokea shukrani zetu kwa yote uliyofanya. Katika Jina la Yesu Kristo tunatazamia baraka Zako. Amina.

Mnaweza kuketi.

2 Na, vema, ni—ni baridi kidogo tu Jumapili hii usiku, hapa ndani, kuliko ilivyokuwa Jumapili iliyopita usiku. Tunawashukuru sana ndugu zetu waliofanya kazi kwa uaminifu sana kuleta jambo hili. Ninajua wawili ama watatu wao. Ndugu Mike Egan, ninapona huko nyuma, nami ... Ndugu Mike, na Ndugu Sothmann, Ndugu (ninaamini) Roy Roberson, na Ndugu Woods, na hao wote, walikuwa hapa chini wakitokwa na jasho tu, wakijaribu kuiingiza kusudi tupate Ujumbe huu sasa, ama leo. Kwa hiyo, tunashukuru.

3 Sasa, Jumapili ijayo asubuhi, Bwana akipenda, ninataka kuwa na ibada ya uponyaji, maombi kwa ajili ya wagonjwa. Nasi tutaitenga kwa ibada ya uponyaji, Bwana akipenda.

Niliona, asubuhi ya leo, kuna lundo la lesu hapa. Niliziomba. Nami, mlipokuwa mnaomba na kuimba, niliomba kwa ajili ya lesu; na halafu kuna nyingine hapa usiku wa leo. Kwa hiyo, tu—tunaamini ya kwamba Mungu huwaponya wagonjwa. Kuna shuhuda nyingi sana za uponyaji miongoni mwetu, na kote ulimwenguni, nasi tunashukuru kwa ajili ya jambo hili.

Nami nilifikiri, Jumapili ijayo, kwa kuwa sina budi kuondoka kwa muda kidogo, na tumekuwa tukishikilia sana mafundisho na Ujumbe, hata nilifikiri lingekuwa jambo zuri kama tungekuwa na—na ibada ya uponyaji, tukawaomba wagonjwa. Nasi tunatumaini ya kwamba Mungu atatupa wakati mzuri sana.

4 Sasa, wengi wenu inawabidi kuendesha magari maili nyingi usiku wa leo. Kwa hiyo nilikuwa nikizungumza na makundi kule—kwenye Mkahawa wa Blue Boar, leo, ambapo nilikuwa nikila chakula cha jioni. Watu wengi wazuri, sina budi kuwapa mikono na kuzungumza nao, watu ambao sijawahi kukutana nao hapo awali, wanaokuja hapa kanisani. Nami ninashukuru kwa ajili ya marafiki kama hao, nami ninataka kumshukuru kila mmoja wenu. Baadhi yao wamechuma forsadi nyeusi, na kutuletea. Na mmoja akatuletea ndoo ya asali, ama molasesi, naamini ilikuwa hivyo, na—na mambo tu. Hujui hilo linamaanisha nini. Na asubuhi moja, naja huku na kutoka nyumbani, wakati mwingine kule ...

5 Asubuhi nyingine kulikuwa na ndugu fulani pale ambaye alikuwa na hali mbaya sana, hakuwa na nguo na kadhalika, alitaka niende nikamletee nguo chache. Nikaanza kutoka, nami karibu niikwae kwenye ndoo ya forsadi nyeusi iliyokuwa pale. Nikasema, "Je! ni wewe ulieleta hizi forsadi nyeusi?"

Naye akasema, "La, kamwe sihusiki kabisa nazo. Nimekuwa hapa kabla ya mapambazuko, na zilikuwa hapa wakati huo." Na ilikuwa Ndugu yangu mwema Ruddell alikuwa ameniletea. Na, kwa hiyo, mambo hayo hakika ninayathamini.

Billy Paul ndiyo kwanza anigusie, dakika chache zilizopita, ya kwamba miongoni mwa kusanyiko hili usiku wa leo, walikuwa wametoa sadaka, hiyo kwa ajili yangu. Na—nawashukuru kwa ajili ya jambo hilo. Sikutaka mfanye hivyo. Ni—ninathamini sana jitihada zenu, na kadhalika, lakini hilo jambo halikuwa la lazima. Na, lakini, Bwana awabariki. Mnajua, mnajua, Biblia ilisema, "Kadiri mlivyomtendea aliye mdogo sana wa hawa, mlinitendea Mimi."

6 Sasa, kwa namna fulani nimekuwa nikizungumza nanyi, juu ya Ujumbe, moja kwa moja. Nami ... Watu wengine wanaweza kuwa na mawazo ya kwamba—ya kwamba nafikiri ya kwamba Yesu atakuja asubuhi ama usiku wa leo. Ninaamini hivyo. Sasa, sisemi ya kwamba Yeye atakuja. Na, tena, Yeye huenda asije kwa juma lijalo, na huenda ikawa ni mwaka ujao, huenda ikawa ni miaka kumi. Sijui Yeye atakuja lini. Lakini, kuna jambo moja ninalotaka kuninii ... daima kumbukeni, mwe tayari kila dakika ama saa. Mnaona? Kwamba, asipokuja leo, huenda akawa hapa kesho. Kwa hiyo weka tu hilo niani mwako, ya kwamba Yeye

yuaja.

Nami sijui ni wakati gani utakuwa saa yangu ya mwisho hapa duniani, wala ye yote wetu hajui. Na hakuna mmoja wetu ajuaye Yeye atakuja lini. Hata hajui, Mwenyewe, kwa Maneno Yake Mwenyewe; Yeye alisema, "Baba, pekee, ndiye ajuaye Yeye atakuja lini; hata Mwana hajui atakapokuja." Ni wakati Mungu anapomtuma kwetu tena. Lakini tunatazamia Kuja Kwake. Na kama Yeye haji katika kizazi changu, Yeye anaweza kuja katika kingine; kama Yeye haingii katika hiyo, Yeye atakuja kingine. Lakini, kwangu mimi, ni vigumu kuona wakati wowote uliosalia. Ninaninii tu ... Kwangu mimi, lingeweza kutukia dakika yoyote. Sasa, hilo halimaanishi ... Hilo halimaanishi, sasa, ya kwamba mtaona mbingu zikibadilika na kila ... Huko siko kule Kuja ninakozungumzia. Ninazungumza juu ya Kunyakuliwa.

7 Unaona, Yeye anatembea kuja mara tatu. Yeye alikuja katika majina matatu ya wana. Yeye alikuja katika utatu; Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Mnaona, yote ni Kristo yule yule, Mungu yule yule, wakati wote. Sasa, tunajua Yeye alikuja kuleta kazi tatu za neema; kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kila kitu, katika Mungu, kinakamilika katika tatu.

Na kwa hiyo Yeye alikuja, kwanza, kumkomboa Bibi -arusi Wake. Yeye anakuja, pili, kama Kunyakuliwa, kumwondoa Bibi-arusi Wake. Yeye anakuja, wa tatu, pamoja na Bibi -arusi Wake, Mfalme na Malkia; baadaye, hapo ndipo watu wengi wanapotarajia kule Kuja.

Lakini wakati atakapokuja wakati huu, hakuna hata mmoja ila wale walio tayari watajua wakati atakapokuja. Kutakuwako na kukosekana tu kwa watu. Hawatajua kilichowapata. Watanyakuliwa tu, katika dakika moja, na kwamba watapotea tu. "Kubadilishwa katika dakika moja, katika kufumba na kufumbua." Kwa hiyo uwe tu tayari kwa ajili ya jambo hilo. Lingekuwa ni jambo la kutisha sana asubuhi moja kumkosa mpendwa, hakuna mtu anayeweza kuwapata. Si ingekuwa ni vibaya sana kujua umekwisha kupita na ukakosa? Kwa hiyo jiweke tu mbele za Mungu.

8 Sasa, juma lijalo, Bwana akipenda, Jumatatu ijayo, juma moja kuanzia Jumatatu hii, Mungu akipenda, ninairudisha familia huko Arizona ambako wanaenda shuleni, ndipo ni—nitarudi.

Sasa, siendi huko nje ... Sina huduma zozote za kuwa huko nje. Ni vigumu kwangu kuwa Arizona. Huondoka nikaenda mahali pengine. Ninampeleka mke wangu kule, Jumatatu ijayo. Ninarudi hapa tena. Nitaondoka hapa niende British Columbia. Nitarudi Colorado. Nitakuwa Arizona tena wakati mwingine karibu na Krismasi, kwa dakika chache tu, kwa muda wa kutosha ... labda siku mbili au tatu, nitaikusanya familia, nitarudi hapa kupitia likizo ya Krismasi, Bwana akipenda, kuwa na ibada katika juma la mwaka mpya hapa .

9 Kwa hiyo basi niko hapa, kwa kweli, zaidi. Niko hapa mara kumi zaidi ya huko nje, kwa sababu hatuna kanisa lo lote wala ibada yo yote kule, hakuna kitu tulicho nacho huko nje, kwa hiyo, kwa namna fulani ya ibada ya kanisa. Hilo ndilo jambo moja baya juu yake. Sina mahali pa kuwatuma watoto ambapo watakaosikia Ujumbe huu, kama vile watoto wenu wanavyosikia hapa, na—na kwa hiyo hiyo ni kasoro moja tuliyo nayo. Lakini wote wana afya zaidi. Hali ya hewa ni kavu, joto, kavu, lakini watoto wote wanaonekana wana afya nzuri zaidi. Mimi sikai huko vya kutosha kujua kama ni pana afya ama hapana. Mimi, niko safarini, na ni—ni—nadhani nilizaliwa tu mzururaji.

Mke wangu huniita ... Mke wangu huniita...Najua yuko hapa, kwa hiyo nitajuta jambo hili baada ya kanisa, nyote mwajua. Hiyo inaitwaje, pepo zinazohamama, ama pepo zisizotulia, ama cho chote—cho chote kile, mwajua, mchanga wa kuhamama? Ama, mimi daima situlii, kwa maneno mengine. Nami nimeoa sasa, miaka ishirini na miwili, nami, wakati mwingine, nami wakati mwingine hufikiri ni mgeni nyumbani, kwa sababu sina budi kuondoka.

Lakini ninatazamia wakati ambapo tutatulia katika ile Nchi ya nyumbani siku moja. Lakini sasa vita vinaendelea, kwa hiyo hebu na tuwe katika maombi.

10 Usisahau, Jumapili ijayo asubuhi, Bwana akipenda, waleteni wagonjwa wako na wanaoteseka. Njooi mapema, chukuani nafasi zenu, na labda kuna kundi litaloombewa. Itatubidi kutoa kadi za maombi. Kama hakuna wa kutosha, hatutatoa kadi za maombi, za kutosha tu kuunda mstari mdogo kama dazani mbili ama tatu, ama chochote kile. Lakini sisi—labda tutatoa kadi za maombi, kwa hiyo labda tutafanya hivyo saa moja kabla ya ibada ya kawaida, ambayo nafikiri huchukua ... Itakuwa ni saa mbili, saa mbili au saa mbili na nusu, watatoa kadi za maombi; fungua kanisa, kutoa kadi za maombi Jumapili ijayo asubuhi. Na halafu hakikisheni mtakuwa hapa kwa ajili ya ... Waleteni wapendwa wenu, wawekeneni mle. Itakuwa hali nzuri na ya baridi kanisani, kama wao ni wagonjwa, nasi tutafanya kila tuwezalo kuwaombea.

Asanteni, tena, kwa ajili ya sadaka ya upendo.

11 Na sasa tutasoma kidogo Neno la Mungu, usiku wa leo, na tuwe tayari kwa tukio hili la Uwepo Wake tena kutuletea Neno Lake. Sasa, tunajua tunaweza kusoma somo, bali Mungu hana budi kufunua muktadha. Mnaona? Tunaweza kuchukua somo, bali Mungu hana budi kufunua muktadha. Na wakati mnapofungua sasa katika Kitabu cha Yeremia, mlango wa 2.

Ninataka kusema ya kwamba ninafurahi kuwa, pamoja nasi, Ndugu Lee Vayle, ndugu mpendwa katika Bwana. Nami nafikiri hapa, ndugu hapa, siwezi kukumbuka jina lake, Ndugu Willard Crase. Nami niliwaona ndugu kutoka Arkansas, Ndugu John na hao wengine, kutoka karibu na poplar Bluff, na Ndugu Blair. Na, loo, Ndugu Jackson, na Ndugu Ruddell, na wengi sana ambao si—siwezi ... Laiti ningaliliita jina la kila mtu, bali siwezi kufanya hivyo, nanyi mwafahamu. Ndugu Ben Bryant, ninamwona ameketi hapa; yeye kwa kawaida ndiye kona yangu ya amina ninapokuwa ... Kila mtu anamjua Ben kwa sauti yake. A-ha.

12 Sisi, tukiketi California wakati mmoja, nilikuwa nikihubiri Ujumbe kwa ajili ya Wabaptisti kule bondeni. Walikuwa na hema kubwa pale, na Wabaptisti wengi wa tabaka la juu. Singeweza kamwe kusikia "amina" kutoka mahali popote; mnajua, wakihofu baadhi ya wanawake wataharibu vipodozi nyusoni mwao. Halafu basi, muda si muda wajua, niliona jozi ya miguu kama hiyo, ikienda hewani, na mikono miwili mikubwa, na nywele nyeusi zikitikiswa pale, zikipiga makelele, "Amina," zikipiga makelele namna hiyo. Nami nikaangalia chini, nikasema, "Ben, ulitoka wapi?" Yeye kweli alikuwa akisema "amina."

Ninamwona mke wake akimwalia, kidogo. Vema, yeye anapoteza kidogo hizo nywele nyeusi, lakini hiyo ni sawa, mwajua. Usifadhaike juu ya jambo hilo. Nilifanya hivyo, zangu, muda mrefu uliopita.

Kwa hiyo, sasa, msisahau kuomba.

13 Sasa wakati tunapofikia upande wa uaminifu wa ibada, kumbukeni, kama tukisoma Neno hili, basi Mungu atalibariki Neno Lake. "Halitamrudia bure, bali litatimiza yale yaliyokusudiwa." Nami ninajua, katika kusoma Neno, daima nitakuwa sahihi. Ninapolisoma Neno, Mungu ataliheshimu Neno Lake.

Sasa hebu na tusimame kwa heshima ya Neno Lake. Yeremia, sura ya 2, aya ya 12 na 13 ya Yeremia 2.

*E-...mbingu, staaabuni kwa sababu ya jambo hili, mkaogope sana, na kuwa na ukiwa sana, asema BWANA.*

*Kwa maana watu wangu hawa wametenda maovu mawili; wameniacha mimi, niliye chemchemi ya maji ya uzima, wamejichambia mabirika, mabirika yavujayo, yasiyo-... yasiyoweza kuweka maji.*

Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa.

14 Mungu mpenzi, Neno Lako limesomwa. Nasi tunaomba ya kwamba Wewe utaliheshimu Neno hilo na utupe leo mfano ama kifani Chake; huku tunapoangalia siku zilizopita, Israeli, kama mfano, kama Biblia inavyotufundisha ya kwamba tunaweza kuona uliyowatendea wakati walipolitii Neno, tuone ulivyowafanyia walipokosa kuliadini Neno, na tujue litupasalo kufanya. Kwa hiyo, tunaomba ya kwamba utazungumza nasi usiku wa leo kwa njia ya pekee sana, tupate kujua jinsi ya kujiendesha katika siku hii, ambayo tulijifunza asubuhi ya leo tunayoishi. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Huenda mkaketi.

15 Ninataka kuzungumza usiku wa leo juu ya somo hili, kwa—kwa muda mfupi tu juu ya: Mabirika Yavujayo.

Israeli walikuwa wamefanya maovu mawili makubwa. Mungu alisema walikuwa wamemwacha Yeye, Chemchemi ya Uzima, nao walikuwa wamejichambia mabirika ya kunywea. Sasa, hilo ni jambo fulani.

Sababu ya mimi kufikiria juu ya somo hili ilikuwa ni kwa sababu ingeenda sambamba na yale niliyokuwa nikisema asubuhi ya leo, ya saa tunayoishi, na Sababu tunayoshindania.

16 Nasi tunawaangalia Israeli kama mfano, kwamba, kile Mungu alichokuwa, daima hana budi kubaki vile vile. Na kuna jambo moja tu ambalo Mungu aliwahi kuheshimu, hilo lilikuwa, njia Yake ambayo aliandaa kwa ajili ya watu. Na wakati walipotoka nje ya njia hiyo, basi Mungu alitahayarishwa, na Mungu akawafanya watu wateseke kwa ajili ya kuyaacha yale aliyokuwa amewaambia wafanye, haidhuru ilikuwa ni nini.

Yeye hata aliwapa sheria, "Usiguse, usishike, usionje." Si tu kwa sababu ya uovu wa kufanya jambo hilo, bali uovu wa kutotii yale Yeye aliyosema wafanye. Na daima hakuwezi kuwa na sheria bila adhabu kwa sheria. Kwa sababu, kama hakuna adhabu, basi, sheria si muhimu kwake isipokuwa iwe na adhabu. Torati!

17 Sasa, tunaona, yale waliyofanya katika siku hiyo yanaonekana sambamba na yale tunayofanya leo, yale watu wa kanisa wanafanya.

Sasa tunaona jambo la ajabu hapa. Huenda likawa ni jambo geni kwa watu fulani, wakati Yeye aliposema, "Ninyi, wao, wamejichambia mabirika, mabirika yavujayo." Sasa, labda baadhi yenu hamjui birika ni nini. Ni wangapi wanaojua birika ni nini? Vema, karibu ninyi nyote. Kama uliwahi kulelewa

shambani, unajua birika ni nini. Ninakumbuka nimekunywa wadudu wa kutosha kutoka kwenye moja, ku—kujua nini—ninii birika.

Nimehubiri nchini ambapo, kwenye miti ya vivuli, ambapo ungekuwa na mtungi mkubwa wa maji ya birika uliowekwa pale, nje ya—ya mvua, mwajua, na kwa namna fulani yalika sana. Na—na halafu wadudu, wakati wa usiku, wangeingia mle. Na kwa hiyo ninajua maji ya birika ni nini.

18 Bi—birika ni—ni mahali, kitu kilichochimbwa ardhini, kuchukua mahali pa kisima. Ambapo watu hawana kisima, basi wanapata bi—birika. Kwa maneno mengine, birika ni tangi la kujitengenezea ama kisima kilichotengenezwa na mwanadamu ardhini, ambacho mtu anachimba, kuchota maji, ku—kuyatumia. Baadhi yao huyatumia kwa maji ya kuoshea, na wengine huyatumia kama maji ya kunywa, na kwa njia mbalimba, labda. Maji yote wakati mwingine, tuliyozea kuyapata, yalikuwa kwenye birika. Tulikuwa na kitu cha kale ambacho ilikubidi kuzungusha, na kuzungusha, na kuzungusha, na kuzungusha, na kuzungusha, kuyavuta maji; kilifungiwa ndoo ndogo, kuyavuta maji hayo kutoka kwenye hilo birika.

Vema, tunaona jambo moja kuhusu birika ambalo ni tofauti na kisima. Sasa, birika litakuwa tupu. Bi—bi—birika haliwezi kujijaza lenyewe. Ni—ni ... Halitumainiki. Huwezi kutumainia birika. Halina budi kutumainia na kutegemea mvua zinazonyesha katika majira ya kiangazi ama katika majira ya kipupwe, vyovyote itakavyokuwa ... Kwa kawaida, katika majira ya kipupwe wakati theluji na mvua zinapokuja, basi maji hutiririka kwenye birika. Na kama halipati maji hayo, basi hu—huna maji yoyote. Yote—yote ... yanakauka. Wala haliwezi kujijaza lenyewe. Birika hilo la kale haliwezi kujijaza lenyewe. Linapata kujaa kwake kutokana na—na mvua zinazonyesha.

19 Nami nawatakeni mwone jambo lingine kuhusu birika. Kwa kawaida, unaona, ama jinsi ilivyokuwa mahali petu, birika ... Kwa kawaida ghala huwa karibu ukubwa wa nyumba mara mbili, na kwa kawaida wao huyaelekeza maji ya hayo kutoka kwenye hilo ghala, kwenda kwenye birika. Ninakumbuka kile kisima cha kale kilichokuwa huko nje, wakati alipokuwa ... wakati ma—mabomba ya kutolea maji yanaingia ndani yake, pia, kutoka kwenye lile ghala. Hujaza kutoka ghalani.

Kwa hiyo basi maji yanatolewa kutoka kwenye hilo paa la ghala; ambapo, wanyama wote wanakanyaga-kanyaga kila mahali kwenye uwanja wa zizi, na kila taka ya uwanja wa kibanda hicho inakaa juu ya ile ghala ya nafaka, katika nyakati za kiangazi. Halafu maji yanakuja na kuifagia yote toka paani, yakaingia katika kihori ambacho ni cha kujitengenezea, kisha yakaingia kwenye mfuko wa maji wa kujitengenezea, mpaka kwenye birika la kujitengenezea. Na kama huna takataka, sijui una nini, unapokuwa na birika. Naam, bwana! Lote ni ya kujitengenezea, na ni chafu tu yawezavyo kuwa.

20 Mwajua, tulizoea kuiita ... Tulikuwa na kitambaa cha kuchujia kwenye moja. Je! Uliwahi kujua hicho kilikuwa ni nini? Ilitubidi kuweka kitambaa cha kuchujia juu yake, kuzuia wadudu wote na vitu vilivyotoka juu ya lile—lile ghala la nafaka, na kuzunguka mahali pale; na kuyamwaga kutoka mahali pamoja hadi pengine, hata kwenye birika. Nasi tulikuwa tunaweka ki—kitambaa cha kuchujia juu yake, kuzuia ta—taka zote za juu na kadhalika ambazo tuliweza. Bila shaka, hicho hakingaliweza kushika taka yenyewe, ilishika vitu vikubwa vilivyoshuka na kuangukia ndani yake. Huenda mdudu akaanguka mle ndani, bali utomvu wa mdudu huyo ulichukuliwa na maji. Kwa hiyo, kwe—kweli ulikuwa na uchafu hapo ulipokuwa na birika chafu la kale.

21 Kwa hiyo, kwe—kweli ulikuwa na uchafu hapo ulipokuwa na birika chafu la kale. Ukiyaacha maji hayo yasimame kwenye birika, yanakuwa maji yaliyooza. Ndipo yanajaa—yanajaa vyura, na mijusi, na nyoka. Nasi tulizoea kuwaita “vifurukuta-mikia,” ninii wadogo... Sijui kama ... Wao si kimelea, wao ni ... Siwezi, sijui ungewaitaje. Bali vitu vidogo vinaingia majini, ambavyo tuliita vifurukuta-mikia. Mnajua ni kitu gani. Ni wangapi wanaojua ninachozungumzia? Loo, mbona, bila shaka, nyote mnaotoka mashambani mnajua. Mkiyafanya kuoza sana, na basi hawa wanaopenda maji yaliyooza wanaambatana nayo. Kwa kweli huja tu, kwa sababu maji yameoza. Na kwa sababu yameoza, yanawavutia wanyama mle wanaopenda vitu vilivyooza.

22 Na hiyo ni kama makanisa yetu siku hizi. Nafikiri kwamba tumeacha ... Moja ya dhambi kubwa mno ambazo makanisa yametenda leo, kama Israeli wakati huo, yalimwacha Yeye, Chemchemi ya Maji ya uzima, na kujichimbia mabirika ya kujitengenezea. Nayo yanakuwa makao ya kila kitu kinachopenda maji ya namna hiyo. Mijusi, vyura, na viini vichafu vya kila namna, vinaishi mle ndani, kwa maana ni tanki la kujitengenezea. Na katika tanki hili ambamo vitu hivi vinaishi, ni mfano mkamilifu wa madhehebu yetu leo.

“Sasa,” unasema, “Ndugu Branham, kwa nini unawashambulia sana watu hao?”

Inapaswa kuwashambulia. Haina budi kushambuliwa. Yatorokeni, kwa maana hatimaye yatafanyika ile alama ya mnyama. Kumbukeni, hiyo ni Kweli! Yatakuwa ni alama ya mnyama. Madhehebu yataongoza moja kwenye kitu hicho. Yamo njiani yakielekea kule sasa, kulazimisha, kwa kutumia nguvu.

Angalia katika milki ya kale ya Kirumi. Jambo hilo ndilo hasa liliwaongoza kwenye ile alama ya ukengeufu. Mliona ya kwamba hakuna mtu angeweza kununua wala kuuza bila alama ya mnyama. Ilimbidi

awe nayo.

23 Kuna tabaka mbili tu za watu watakaokuwa duniani; wale walio na Muhuri wa Mungu, na wale walio na alama ya mnyama. Tabaka mbili tu, kwa hiyo itakubidi kuwa na moja ama nyingine. Na itakuwa ukengeufu, a—alama ya—ya dini, dini kengeufu.

Na itakuwa na alama ya mnyama. Tunaposoma, tunaona ya kwamba Rumi ilikuwa, ndivyo ilivyo, na daima itakuwa, yule ... au, yule mnyama. Kweli kabisa. Hakuna njia ya kuipa kitu kingine chochote. Rumi!

Na Rumi ilifanya nini? Na Rumi ilifanya nini? Ilibadilika toka Rumi ya kipagani ikawa Rumi ya kipapa, kisha ikaunda madhehebu, madhehebu ya dunia nzima, ambayo yalimlazimisha kila mtu kujiunga na dini hiyo la sivyo atawawa.

24 Na ni jambo la ajabu ya kwamba hii Marekani inajitokeza jukwaani, nayo ni kama mwana-kondoo. Na mwana -kondoo ana pembe mbili ndogo, haki za kiraia na za kidini. Na baada ya muda kidogo, wakati hiyo ilikuwa mwana-kondoo, tuliona kwamba ilinena kama lile joka na kutumia uwezo wote wa lile joka la kwanza kabla yake. Na Biblia inatwambia ya kwamba walisema, "Na tumfanyie sanamu yule mnyama." Sanamu ni kitu mfano wa kitu kingine. Nasi tunaweza kuliona sasa hivi, katika hali yake ya ukengeufu, kanisa likiunda Baraza la Makanisa Ulimwenguni, ambalo ni sanamu ya nguvu za Rumi; na litawalazimisha watu kitu kile kile Rumi ya kipagani ilichowalazimisha...ama Rumi ya kipapa ilichowalazimisha. Kwa hiyo, hakuna njia nyingine, hakuna kitu kingine. Lakini hiyo ni Kweli.

Na hiyo ndiyo sababu ninayashambulia katika siku zangu, katika wakati wangu, kwa sababu hayana budi kushambuliwa. Ule mwito ulikuja, kwamba, "Tokeni kwake, enyi watu Wangu, msizishiriki dhambi zake!"

25 Naam, ninayalinganisha hayo na haya mabirika machafu na yenye vinyaa. "Yeye ni Ndiye Chemchemi ya Uzima. Yeye ni Maji ya uzima." Nao watu wanayaacha hayo, na kujichimbia mabirika ambayo yanaweza tu kuteka vinyaa. Hicho ndicho tu yanayoweza kuteka Hicho ndicho tu yanachoweza kuteka. Na hivyo ndivyo umadhehebu unavyofanya; unashika kila kitu kinachokuja na kinataka kujiunga nayo. Yako tayari kukichukua mradi kina pesa ama kinaweza kuvalia kwa namna fulani. Haidhuru wao ni akina nani, wanatoka wapi, wanawachukua, hata hivyo.

26 Sasa tunaona, tena, ya kwamba, hii alama ya mnyama iliyoundwa hapa. Marekani, ni namba kumi na tatu. Ilianzishwa na koloni kumi na tatu. Ilikuwa na bendera iliyokuwa na nyota kumi na tatu, milia kumi na mitatu. Na hata inaonekana katika Ufunuo sura ya 13. Na Marekani daima imekuwa ni mwanamke, aliyewakilishwa kwenye sarafu zetu. Hata kile kichwa cha Kihindi, kwenye sarafu, kina sura ya mwanamke. Tunajua jambo hilo, tunajua historia yake. Kila kitu, Kengele ya Uhuru, na cho chote kile, uhuru ... Sanamu ya Uhuru ni, kila kitu, mwanamke. Mwanamke; namba kumi na tatu. Mnaona? Sasa, ni—ni vizuri kuona mambo hayo.

27 Na sasa nimebashiri kwa ufunuo kutoka kwa Mungu, ama ono katika mwaka wa 1933, ya kwamba mambo saba yangetukia kabla ya wakati wa mwisho. Na kwamba, moja ya hayo, ya kwamba, "Mussolini," ambaye wakati huo alikuwa anaanza kuwa dikteta, "atakuwa dikteta. Na, pia, angefanya uvamizi na kushuka kwenda Ethiopia, na angeiteka Ethiopia. Naye Roho, Yeye alisema, 'Ataanguka katika hatua zake.'"

Sijui kama kuna ye yote wa watu wa kale ambaye amebaki katika Maskani haya, anayekumbuka nikisema kule katika Ukumbi wa Redman huku chini tulipohubiri, miaka mingi, mingi sana iliyopita. Yupo mmoja humu jengoni, usiku wa leo, ambaye amesalia kutoka wakati ule kule kwenye Ukumbi wa Redman nilipohubiri jambo hilo, wakati N.R.A ilipojitokeza, huko nyuma kabisa katika kipindi cha kwanza cha Roosevelt? Nadhani hakuna hata mmoja hapa ndani. Yupo mmoja? Naam, naam, mmoja, kuna mmoja. Naam, Bibi Wilson, ninamkumbuka. Mke wangu, anayeketi huko nyuma. Wamesalia wawili, kutoka kwenye kizazi cha kale cha watu hao katika siku hiyo.

Kwamba, waliposema hii N.R.A. ilikuwa alama ya mnyama, nilisema, "Hakuna kitu kwake; hata kidogo. Alama ya mnyama haiji hapa. Inatoka Rumi. Wala haiwezi kuwa alama ya mnyama."

28 Na sasa kumbukeni ya kwamba mambo haya yalisemwa. Kasema, "Adolph Hitler angefikia mwisho wa ajabu. Naye angeitangaza vita dhidi ya Marekani. Nao wangejenga kitu kikuu—ki—kikubwa cha saruji, hata wangeishi humo ndani yake. Na papo hapo Wamarekani wangepigwa vibaya sana, kwa jambo hili." Na ilikuwa ni ile boma ya Siegfried, miaka kumi na moja kabla hata haijaanza kujengwa. Na kisha akasema, "Lakini angefikia mwisho; na Marekani ingeshinda hivyo vita."

Kisha akasema, ya kwamba, "Kuna itikadi tatu; Unazi, ufashisti, na ukomunisti." Nami nikasema, "Yote yataishia katika ukomunisti. Urusi itazichukua zote, katika ukomunisti."

Nami nikasema, "Basi sayansi itakuwa kubwa sana, mwanadamu atakuwa mwerevu sana, hata atavumbua mambo mengi sana hata atatengeneza motokaa inayoonekana kama yai, ambayo itakuwa na

kitu kama kioo. juu yake, na ingeendeshwa na nguvu nyingine zaidi ya usukani." Nao wana hiyo motakaa.

29 Nami nikasema, "Kisha uadilifu wa wanawake wetu utashuka katika mambo ya aibu sana, hata watakuwa ni aibu kwa mataifa yote. Watavaa nguo za wanaume. Wao wataendelea kuvua nguo zao mpaka wafikie mahali ambapo wana nguo zao za ndani, hivyo tu. Na, hatimaye, watafikia kuvaa tu jani la mtini."

Na kama ukiangalia, katika gazeti la Life la mwezi uliopita, walikuwa na mwanamke aliyevaa majani ya mtini. Na hiyo ni nguo mpya ya jioni, au gauni, wanayovaa jioni; wazi, unayoweza kuona kupitia kwake, ni majani ya mtini tu yanayoficha tu sehemu fulani la mwili wake; bila kamba, au na kamba, nguo za kuogelea zisizo na ukanda, upande wa juu, mwili ulio wazi. Na jinsi ambavyo mambo hayo yametukia!

Ndipo nikasema, "Nilimwona mwanamke akisimama Marekani, kama malkia mkuu ama kitu fulani. Naye alikuwa mrembo sana, lakini mwovu moyoni mwake. Naye akafanya taifa lipige hatua, lifuate nyayo zake."

30 Ndipo nikasema, "Hatimaye, Yeye aliniambia niangalie Mashariki tena. Na, nilipofanya hivyo, niliona, ilionekana kana kwamba, kama ilivyokuwa, ulimwengu ulikuwa umelipuka. Na umbali nilioweza kuona, hakukuwa na kitu ila vijiti, na—na miamba iliyokuwa inafukizia moshi ilikuwa imelipuliwa kutoka ardhini."

Na haya yalikuwa yatendeke kabla ya mwisho wa ulimwengu. Na matano ya hayo saba tayari yametukia, katika miaka thelathini na mitatu. Tuko hapo, tumerudi kwenye wakati wa mwisho!

Nami nilinena dhidi ya mfumo huo wa kimadhehebu papo hapo. Nami bado ninaamini, usiku wa leo, ya kwamba ni shimo la maji machafu, ya kwamba ni mahali ambapo uchafu unatiririkia ndani yake. Siwezi kuamini ya kwamba Mungu angechukua kitu kama hicho katika Kanisa Lake, kwa sababu hakina budi kuzaliwa kwa Roho wa Mungu na kisha kisafishwe kabla hakijaitwa Chake. Mwili wa siri wa Kristo, tunabatizwa ndani Yake kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu.

31 Naam, mfumo huu wa birika bila shaka ni mfano mkamilifu wa madhehebu. Mtu mwenye hekima anapaswa kuangalia, na kamwe asiingie ndani yake, kwa kuwa Mungu amethibitisha kupitia nyakati zote kwamba Yeye anapinga jambo hilo na kamwe hakufanya kazi nalo. Kundi lolote ... Wakati wo wote mtu alipoinuka na ujumbe, kama vile Luther, Wesley, ama kadhalika, na Smith, na Calvin, na hao wengine; wakati walipoanzisha madhehebu, Mungu aliweka kitu hicho kwenye mashelfu na hakukizuru tena katika ufufuo.

Angalia katika historia. Hapajakuwa na wakati ambapo Mungu alipata kuchukua madhehebu, akafanya uamsho kutoka kwake, mahali po pote. Halafu, katika historia na kwa Biblia, inathibitisha ya kwamba ni kitu kichafu machoni pa Mungu, kwa hiyo sitaki uhusiano wowote nacho. Na hiyo ndiyo sababu ninapinga. Ninajaribu kuwaondoa watu humo.

32 Tumealikwa, kama vile katika Israeli, ndivyo ilivyo sasa, kuiangalia Israeli kwa mifano. Wao, mradi tu walikaa na Chemchemi hiyo, walikuwa sawa. Lakini walipoanza kujichimbia mabirika, mifumo ya kujitengenezea, basi Mungu aliwaacha kabisa. Yeye atatufanyia vivyo hivyo. "Wamemwacha Yeye, Chemchemi ya Maji ya uzima." Hayo ndiyo malalamiko ambayo Mungu alikuwa nayo dhidi yao. "Kufanya kitu ambacho wangeweza kusema, 'Mnaona yale tumefanya!'"

33 Sasa, katika wakati wa sa—safari ya Musa; wakati Mungu, kwa neema, alikwishawapa nabii, alikwishawapa ile Nguzo ya Moto iwatangulie, akaithibitisha kwa ishara na maajabu. Neema ilikwishatoa vitu hivi vyote. Israeli bado walitaka, waliona sheria. Walikataa neema, kuchukua sheria.

Hivyo ndivyo hasa watu wanavyofanya siku hizi. Wao wanalikataa Neno, kuchukua mfumo wa kimadhehebu, kwa sababu katika jambo hilo wanaweza kufanya watakalo na bila kizuizi. Bali huwezi kufanya hivyo katika Kristo! Huna budi kuja safi na mng'avu, upate kuwa katika Kristo.

34 Wanakiacha kisima kinachofoka maji, wakaziendea taratibu za kujitengenezea ama birika, ungeweza kuwazia mtu fulani akifanya hivyo? Ungewazia jinsi ilivyo akili ya mtu ambaye angekunywa maji matamu ya kisima kinachofoka maji, kisha ayaache hayo akanywe ya birika la kujitengenezea lenye vyura, na mijusi, na vifurukuta-mikia, na kila kitu ndani yake?

Haionekani kuwa ni jambo la busara kuwa sahihi, bali hivyo ndivyo hasa watu wamefanya. Wameacha Neno, Chemchemi ya kweli ya chanzo na Nguvu za Mungu, kunywa kutoka kwenye mabirika, na kujifanyia mabirika. Kama vile walivyofanya wakati huo, wamefanya hivyo sasa. Wanasema ... Yeye alisema, "Wameniacha." Hapa alisema, hapa katika Yeremia 2:14, ama 13, hasa.

Yeye alisema, "Wameniacha mimi, Niliye Chemchemi ya Maji ya uzima."

35 Sasa, tunaona birika ni nini. Tunaona kile inachokinga. Tunaona jinsi inavyotengenezwa. Ni kitu cha kujitengenezea ambacho kinatoka kwenye paa chafu. Yale maji yanayomwagika chini, hugonga kwenye paa lililo chafu, kisha yanatiririka tu kutoka kwenye paa, yanapitia kwenye kihori cha kujitengenezea, yanapitia kwenye mfuko wa kujitengenezea yakaingia katika tanki la kujitengenezea. Na uchafu wote

unarundikana mle, na vi—viini vya magonjwa, na mijusi, na vyura, na vitu vya ardhini, namna hiyo. Na, tazama, wao ni wanyama walio wachafu; vifurukuta-mikia, maji yaliyooza. Kifurukuta-mkia hakiwezi kuishi katika maji masafi. Kama kikiishi, yangekiua. Hakina budi kuwa katika maji yaliyooza.

36 Na hivyo ndivyo ilivyo na vimelea hivi vingi leo. Humwezi kuishi katika maji safi ya Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo sababu wao wanapinga Neno kwa nguvu, na kusema, "Linajinga Lenyewe. Hakuna kitu Kwake." Ni kwa sababu hawana budi kuwa na namna fulani ya kidimbwi chenye maji yaliyooza kufurukutia mle. Sawa.

Hivyo ndivyo ilivyo na vyura, na kwa mijusi, na kwa viluwiluwi, na vitu kama hivyo. Hawana budi kusogea kwenye bwawa ama kidimbwi chenye maji yaliyooza, wapate kuishi, kwa maana asili yao ni kuishi mle. Wala huwezi kumbadilisha mnyama mpaka ubadilisha asili yake.

Wala huwezi kumfanya mtu alione Neno la Mungu mpaka asili yake imebadilishwa; na wakati asili yake imebadilishwa kutoka alivyo, akawa mwana wa Mungu, na Roho Mtakatifu anaingia ndani yake. Roho Mtakatifu aliandika Neno la Mungu!

37 Leo nilikuwa nikizungumza na rafiki yangu mzuri, Daktari Lee Vayle, ambaye yupo sasa. Naye ni mwanatheolojia kabisa, na kwa hiyo kwa kawaida tuna—tuna mazungumzo mazuri sana juu ya Maandiko. Mwerevu sana.

Naye akaniuliza wakati mmoja kile nilichowazia kuhusu ushahidi wa kwanza wa Roho Mtakatifu, "Je! Ilikuwa ni kunena kwa lugha?" Imekuwa miaka mingi iliyopita.

Nikasema, "La; siwezi kuona hilo."

Yeye alisema, "Wala mimi pia," kasema, "ingawa nimefundishwa jambo hilo." Akasema, "Unafikiri ni kitu gani kingekuwa ni ushahidi?"

Nikasema, "Ushahidi mkamilifu kabisa ninaoweza kuwazia ni upendo." Na kwa hiyo tukaanza kuzungumza juu ya jambo hilo.

Na ndipo nikafikiri hilo lilisikika zuri sana kwa hiyo nilishikilia tu hilo, "Kama mtu ana upendo."

Lakini siku moja Bwana, katika ono, akanisahihisha. Naye alisema, ya kwamba, "Dhihirisho la Roho lilikuwa ni wale walioweza kulipokea Neno," si upendo, wala kunena kwa lugha, bali ni kupokea Neno.

38 Halafu basi Daktari Vayle alikuwa akiniambia, ya kwamba, "Hilo ni Maandiko," akasema, "maana, katika Yohana 14, Yesu alisema, 'Wakati Yeye Roho Mtakatifu atakapowajilia, atawafunulia mambo haya, ambayo nimewafundisha, naye atawaonyesha mambo yajayo.'"

Kwa hiyo kuna thibitisho halisi la Roho Mtakatifu! Hajawahi kuniambia jambo lolote ambalo siyo sahihi. Kwamba, "Ni dhihirisho la Roho Mtakatifu, ni yeye yule anayeweza kuliadini Neno." Unaweza kulipokea.

Maana, Yesu hakusema kamwe, "Roho Mtakatifu atakapokuja, mtanena kwa lugha." Yeye hakusema kamwe, Roho Mtakatifu akija, ungefanya lolote la mambo hayo. Lakini Yeye alisema, "Yeye atachukua mambo haya yaliyo Yangu na kuwapasha habari, na mambo yajayo atawapasha habari zake." Kwa hiyo huo hapo ushahidi halisi wa Roho Mtakatifu, kulingana na Yesu Mwenyewe.

39 Kwa hiyo mihemuko hii yote na kadhalika waliyo nayo watu na wangali wanaishi, unaweza kuona ni kwa nini wanafanya hivyo. Unaona, linakuwa dhehebu, ama kidimbwi chenye maji yaliyooza, na kamwe hakutakuwa na madhehebu yaliyoundwa juu ya ... Neno kamilifu la Mungu. Haiwezekani, kwa maana huwezi ukachagua ama kuunda madhehebu kutokana na Mungu. La, bwana! La, bwana!

Sababu ni kwamba, unapata kundi la watu wanaoweza kuliadini Neno, acha waanzishe madhehebu. Muda si muda, katika kipindi cha mwaka mmoja kuna kundi la akina Ricky mle ndani ambalo usingeweza kufanya chochote nalo. Wao wanashikilia, wala huwezi kufanya lolote juu yake. Si utaratibu wa Mungu. Si wa Mungu, kwa hiyo tunajua ya kwamba kitu hicho hakifai kitu. Kinakuwa birika, na kinakuwa mahali ambapo kila mmoja atapatana juu ya hili, lile, ama lingine, kuwaingiza washiriki mle, ama kuwaacha watu waingie.

40 Tunaona, mfumo huu ulianza wakati mmoja, huko nyuma katika siku za Israeli, wakati walipokuwa wakichimba mabirika haya. Na kulikuwako na mtu mmoja na kundi la Mafarisayo waliokuwa wamechimba mabirika. Nao walikuwa na mtu mmoja jina lake Herode, naye alikuwa mtangazaji, liwali wa jimbo.

Naye akashuka kuja kumsikiliza mtu ambaye hakuchezacheza na madhehebu yao. Yeye alikuwa ni nabii. Na hakuna nabii aliyewahi kuwa na uhusiano wowote na madhehebu, bali aliyachukia. Huyu nabii akaanza kusema, "Msianze kusema ndani yenu, 'Baba yetu ndiye Ibrahimu,' kwa maana nawaambieni Mungu anaweza kumwinulia Ibrahimu watoto katika mawe haya."

Nao wakamleta mtu mashuhuri kumsikiliza. Na huyu mshimiwa alikuwa amemnyang'anya ndugu

yake mke, akamwoa. Na mtu huyo alienda mbele ya uso wake na kusema nini? Walidhani angepatana, na kusema, "Sasa, bwana, wewe, karibu kwenye kiti kizuri hapa. Nawe yakupasa ku ... Nina furaha sana kwamba uko hapa kunisikia leo."

Yohana alienda moja kwa moja mbele yake, na kusema, "Si halali kwako kumchukua." Jambo la kwanza kabisa alilosema, alimkemea kwa ajili ya dhambi yake.

41 Mnaona, madhehebu hutengeneza vidimbwi ambamo mwanamume anaweza kuishi na wanawake, na hao wanawake wanaweza kufanya yasiyofaa, na kukata nywele zao, na kuvaa kaptura, na cho chote kile, na kujiita Wakristo.

Lakini Chemchemi halisi, haleluya, ya Nguvu za Mungu, haiwezi kukaa pale, kwa sababu inaisukuma nje. "Mimi ni Chemchemi ya Maji ya uzima. Waliniacha Mimi, kujichimbia mabirika."

Sasa, chemchemi ya maji ya uzima, tunaona, chemchemi ya maji ya uzima ni nini? Tunaona birika ni nini, sasa chemchemi ya maji ya uzima ni nini? Ni kisima kinachofoka maji.

"Kisima kinachofoka maji, ni kitu gani hicho, Ndugu Branham?"

Ni kisima ambacho daima hutoka chini na kusukuma maji yake nje. Kinatiririka wakati wote. Kinajitegemea. Daima kinaburudisha na safi, kisima cha maji, chemchemi ya maji ya uzima. Hayakufa na kuoza. Yanaishi, yanabadilika kila wakati, yanaleta kitu kipya wakati wote, yakiendelea, yakitoka kwenye vyanzo vyake. Yanatoa nguvu zake kutoka—kutoka kwenye chanzo chake, ambacho ni ... bado ni chemchemi ya maji ya uzima yakinyunyizia. Kinajisafisha chenyewe; ni kisafi, halisi, maji safi. Kinajitegemea; haikubidi kungojea mvua ijaze tangi lake. Daima kinabubujika, kinatoa maji yake bure. Si lazima uyavute kwa mashine, kuyavuta kwa winji, kuyavuta, ama kujiunga nayo. Ni chemchemi tu ya maji ya uzima.

42 Mnajua, mkichukua mabirika haya ya kale, huna budi kuyazungusha, na kuyazungusha, na kuyazungusha kwa mpini, kuyavuta kwa mashine na kila kitu, kusudi upate kuteka maji kidogo ya hayo yaliyooza. A -ha!

Bali Chemchemi ya Maji yaliyo hai huyatoa, bure, bila kuyavuta kwa mashine, kujiunga, cho chote kile. Loo, nina furaha kwa ajili ya Chemchemi hiyo! Naam, bwana!

Haihitaji chujio juu Yake, kutoa vimelea. Kwa kuwa, inakuja kutoka kwenye kina kirefu sana, huko kwenye Mwamba, mpaka hakuna vimelea kule.

Haihitaji kuwa na kitambaa cha elimu kinachoning'inia juu Yake, hiyo ni kweli, mfumo fulani uliotengenezwa wa kilimwengu wa hekima ya kidhehebu ya kujitengenezea; kukwambia, mbele ya mtaalamu wa magonjwa ya akili, kama unaweza kuhubiri au la. Haina moja ya hayo matambara machafu yanayoning'inia juu Yake. Ingezisukumiamwali mara moja unapozitia mle. Huwezi kufanya hivyo. Kisima hicho kinabubujika, wakati wote. Kama ukikivalisha moja ya hayo matambara, kingeyatupilia mbali upande mmoja au mwingine. Hakina wakati wa kuvalia matambara ya kimadhehebu.

43 Hakihitaji chujio, hakihitaji kichujio, hakihitaji kuvutwa kwa mashine, kushtuliwa ghafla, wala cho chote kile. Kiko pale tu, kikibubujika. Hakihitaji kutegemea mvua za mahali hapo kukijaza. Mvua ni "ufufuo," ambapo Chemchemi hiyo ... Ni hapo kwenye ile Chemchemi ya Uzima. "Palipo na mzoga, tai watakusanyika." Haikubidi kuvuta uamsho kwa mashine; haikubidi kuvuta kitu. Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuja tu kwenye Chemchemi. Daima imejaa maji mazuri, safi, wala hayana mwisho. Inaendelea tu kububujika.

Si lazima uende kwenye birika, na kusema, "Vema, kama ikinyesha na maji yatiririke kwenye lile ghala la nafaka, tutapata maji ya kunywa." Mnaona? Jamani, jamani! Si hiki. Hicho kisima kinafoka maji maji mazuri, baridi wakati wote. Unaweza kukitegemea. Haikubidi kusema, "Vema, nitaenda kwenye birika hili la kale. Tulizoea kunywa maji mle, bali mvua haijanyesha muda mrefu. Nakwambia, huenda ikawa imekauka."

44 Hivyo ndivyo ilivyo baadhi ya mifumo hii ya kujitengenezea. Unaweza kuingia mle, kama unendelea kitu fulani kikubwa, kama una shirika fulani la kisiri la kuuza vitu, ama—ama namna fulani ya kitu kinachoendelea, na karamu kubwa na kadhalika vikiendelea, michezo ya kitapeli, na karamu katika orofa ya chini, na kila kitu, huenda ukaipata nyumba imejaa.

Lakini unapoenda mahali ambapo Chemchemi hiyo inabubujika, daima, watu wako kule wakipata kinywaji cha maji mazuri, maji ya baridi. Unaweza kuitegemea! Sema, "Hawajapata ufufuo kwa miaka kumi." Kama unaishi karibu Chemchemi hiyo, siku zote ina ufufuo unaoendelea.

45 Kama vile alivyosema yule maskini Muwelsh. Ama, wakati mmoja wakati ufufuo wa Kiwelshi ulikuwa unaendelea, kulikuwa na watu mashuhuri kutoka Marekani. Baadhi ya hawa Madaktari wakuu wa Uungu walikwenda huko Wales, wapate kujua ni wapi na haya yote yalihusu nini. Kwa hiyo walikuwa wamevaa



kola zao zilizopinduliwa, na kofia zao zenye kizibo, nao walikuwa wakitembea barabarani.

Na huyu hapa maskini polisi anakuja, akiizungusha fimbo yake ndogo mkononi mwake, huku anapiga mluzi, "Pale msalabani alipofia Mwokozi wangu, hapo nililia nipate kusafishwa na dhambi; hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu, Jina Lake litukuzwe," huku anatembea barabarani.

Kwa hiyo wakasema, "Huyu anaonekana ni mtu wa kidini. Tutakwenda kumwuliza."

Nao wakasema, "Bwana!"

Kasema, "Naam, bwana?"

Akasema, "Tuko hapa kutoka Marekani. Sisi ni wajumbe. Tumekuja hapa kuchunguza ufufuo wa Kiwelshi, kama unavyoitwa. Sisi ni Madaktari wa Uungu, nasi tuko hapa kuuchunguza." Akasema, "Tunataka kujua mahali ufufuo ulipo, na mahali unapofanyika."

Akasema, "Bwana, mmeshafika. Mimi ni ndimi ufufuo wa Kiwelshi." Amina! "Ufufuo wa Kiwelshi umo ndani yangu. Umo humu."

46 Hivyo ndivyo ilivyo wakati unapoishi kwa hiyo Chemchemi ya Maji ya uzima. Hayo ni hai siku zote, yakibubujika na kububujika, bubujika na kububujika na tena na tena. Hayana mwisho Wake. Si eti, "Nenda kaangalie kama maji, kama tulipata mvua hapa muda mrefu uliopita," si hivyo. Ni ile Chemchemi ya Maji ya uzima. Kama ninavyosema, Inatoa Maji Yake bure.

Si lazima uweke matambara juu Yake, upate kujua; baadhi ya matambara ya kielimu, kabla hujamtuma aende akahubiri, na uone kama anaandika maneno yake vizuri, anayanena vizuri, kama anatomia majina yake na viwakilishi, na kadhalika, na vivumishi. Wengi wao hata hawajui ni nini, bali yeye anaishi kwenye Chemchemi vivyo hivyo, mnaona, vivyo hivyo.

47 Haihitaji kutegemea mvua za mahali hapo, kuijaza, ama ufufuo wa mahali hapo, kwa ajili yake. Si lazima ifanye hivyo, kwa maana Nguvu zake na usafi wake vimo ndani yake. Humo ndimo Neno lilipo, Nguvu Yake Yenyewe! Wakati mtu anapoweza kulipokea moyoni mwake, lina usafi Wake. Ina nguvu Zake. Iko moja kwa moja katika Neno Lenyewe, inafoka Uzima.

Israeli wangeiacha, wangeingia katika shida. Kila wakati walipoiacha, walipata shida.

Ni kama vile tunavyofanya sasa. Wakati ufufuo unapoondoka kwenye Hiyo, basi haufai kitu. Unajichimbia visima vichache, na, ama mabirika yaliyooza, na huo hapo umekwisha.

48 Lakini Yeye daima aliwasaidia. Kunung'unika kule Bahari ya Shamu, ndipo waliponung'unika ... Hata hivyo, katika yote hayo, Yeye alikuwa amewaahidi, aliwapa ahadi. Alipaswa kuwarudisha papo hapo, jinsi ambavyo tungeliangalia; bali alikuwa ameahidi kuwapeleka kule.

Yeye alifanya nini? Hao wana wa Israeli, Yeye aliwapa Nguzo ya Moto na kila kitu, kwa ajili ya uthibitisho, nabii wao. Nao wakawaongoza kule nje hadi baharini. Na, daima, kuna shida dhidi Yake. Na huyu hapa Farao anakuja na jeshi lake. Nanyi mnajua alilofanya Mungu? Yeye alifungua tu hiyo birika nyekundu, yenye maji yaliyooza.

Bahari ya Chumvi ndicho kitu kilichokufa zaidi ya vyote ulimwenguni. Imekufa kweli. Ina maji yaliyooza. Hakuna kitu kinachoweza kuishi ndani yake.

Naye akaifungua na kuwaweka huru, ng'ambo ya pili. Aliwapeleka mahali ambapo haingewalazimu kufungwa na kitu kama hicho.

49 Huko jangwani, waliona kwamba matangi hayangeweza kutegemewa; yalikuwa yamekauka. Waliona kwamba, walitoka katika shimo moja la maji hata kwenye lingine. Wakati walipokuwa nyikani, walikuwa wakifa kwa njaa, kwa ajili ya kunywa maji. Nao wangeenda kwenye tangi hili hapa, kidimbwi; kilikuwa kimekauka. Walienda mahali pengine; palikuwa pamekauka. Hawangefikiri kabisa watapata maji ya kunywa.

Na kisha mahali pasipotarajiwa kabisa katika jangwa lote, walipata maji. Ilikuwa katika mwamba. Ilikuwa katika mwamba. Mahali pasipotarajiwa kabisa ambapo mtu angepata maji yo yote, ni katika mwamba mkavu katikati ya jangwa. Lakini, unaona, Mungu hufanya mambo kama hayo. Katika mahali pasipotarajiwa kabisa, katika njia isiyo ya kawaida sana. Hilo ndilo tumekuwa nalo daima.

50 Wao wanafikiri huna budi kuyakusanya madhehebu makubwa, pamoja, na uyaache yote yakusanyike pamoja na shughuli nyingi huku na huko, na kadhalika, na kuwashirikisha maelfu, na wote namna hii, kufanya ufufuo.

Wakati mwingine Mungu huchukua maskini jamaa huyo mdogo hata hajui ABC zake, na moja kwa moja miongoni mwa kundi la watu wasiojua kusoma na kuandika ambao ni vigumu kujua mkono wao wa

kulia kutoka kushoto, Yeye anaweza kuinua ufufuo ambao utatikisa ulimwengu. Alifanya hivyo katika wakati wa Yohana. Yeye alifanya jambo hilo katika wakati wa manabii. Hakuna hata mmoja wao, kama tujuavyo, aliyepata elimu, bali Mungu angeweza kuwashika na kufanya jambo fulani nao.

51 Katika Mwamba huu yalitoka maji. Yeye alikuwa Mwamba. Naye akauamuru Mwamba huu, na hauna budi kupigwa. Naye akampa wingi wa maji safi, matamu, mazuri kwa kila mtu aliyetaka kunywa. Yeye aliwaokoa wote ambao wangekunywa Kwake. Sambamba kamili na Yohana 3:16.

*... Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ... kila amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele,*

Mungu aliupiga huo Mwamba, pale Kalvari. Hukumu yetu ilikuwa juu Yake, ili kwamba kutoka Kwake apate kuja Roho wa Uzima ambaye angenipa mimi na wewe Uzima wa Milele. Huo ni mfano Wake mkamilifu, kule jangwani.

52 Haikuwabidi kamwe kuvuta, kuchimba, kusukuma, wala chochote kile; shiriki tu njia Yake aliyoiandaa, bure. Wakati, haikuwalazimu kuivuta juu kutoka kwenye dimbwi la maji. Haikuwabidi kuyavuta juu kwa ndoo. Haikuwabidi kuwa na winchi kuyateka. Iliwabidi tu kuyanywa.

Na hivyo tu ndivyo ilivyo sasa. Haikubidi kujiunga na chochote. Haikubidi kupiga magoti madhabahuni na kuanzisha jambo fulani, kuvuta. Haikubidi kusema neno tena na tena na tena, mpaka utakapopata mchafuko wa lugha. Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kumnywa tu Yeye, bure, njia iliyoandaliwa na Mungu. Hakuna kuvuta, hakuna kusukuma, hakuna kitu; chukua tu Hiyo, bure. Haikulazimu kufanya kitu; Inywe tu. Hiyo ni kusema, iamini Hiyo tu. Hayo tu ndiyo niwezayo kusema juu yake.

Haikuwalazimu kamwe kufanya jambo lo lote kwa ajili yake. Haikuwalazima kamwe kuchimba wayapate. Haikuwalazimu kamwe kupiga magoti na kulia usiku kucha, kwa ajili yake. Waliyanywa tu; ulikuwa umepigwa na ukawa tayari. Hiyo ni kweli.

53 Ninamtazama mtu sasa, anayeketi nyuma ya chumba hapa. Ninakumbuka nikimwambia ya kwamba, kwenye kibanda cha kale cha zizi siku moja, karibu na hori.

Naye akasema, "Lakini mimi sifai."

Nikasema, "Ninajua wewe hufai." Nami nikasema, "Mimi sifai pia." Lakini nilisema, "Unaangalia kile ulicho. Na uache kuangalia kile ulicho, na uangalie Yeye ni nani."

Akasema, "Kama ningeweza tu kuondoa sigara hizi, Ndugu Branham, ni—ni—ningekuwa Mkristo."

Nikasema, "Usiziache. Unajaribu kupata afya kisha unakuja Kwake. Yeye hakuja kamwe kuwaokoa watu wazuri; alikuja kuwaokoa watu wabaya waliojua wao ni wabaya."

Akasema, "Vema ..."

Nikasema, "Sikiza, hutaki kwenda jehanamu, sivyo?"

Akasema, "La."

Nikasema, "Vema, haikubidi kufanya hivyo. Yeye alikufa ili kusudi isikubidi kwenda."

Akasema, "Inanibidi kufanya nini?"

Nikasema, "Hakuna kitu. Ni rahisi tu hivyo."

Yeye alisema, "Lakini kama nikiweza ..."

Nikasema, "Huyoo, unarudia habari za sigara tena. Acha kuwazia juu ya sigara hiyo. Kumbuka tu, wazia juu Yake, yale aliyofanya, kile Yeye alichu; si jinsi ulivyo. Wewe si mwema; na hujakuwa mwema, na kamwe hutakuwa mwema. Lakini, kile alichu, Yeye Ndiye!" Nami nikasema, "Sasa, jambo moja pekee unalopaswa kufanya; kama Yeye alichukua mahali pako kule chini, unakubali tu kwa hiari yale aliyofanya. Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kulikubali tu."

"Mbona," akasema, "hilo ni rahisi. Nitafanya hivyo."

54 Nikasema, "Hiki hapa kijito." Mnaona? Nilimleta hapa na kumbatiza katika Jina la Yesu Kristo.

Baadhi ya watu wake wameketi hapa, nami—najua walinichekelea kwa kufanya jambo hilo, bali nilijua nilichokuwa nikifanya. Niliona ndani ya mtu huyo kitu ambacho kilikuwa halisi. Ningeweza kuona kitu hicho pale, nami nikamchukua na kumbatiza katika Jina la Bwana Yesu.

Na, tulipofanya hivyo, haikuwa muda mrefu baadaye nikaenda nyumbani kwa mwanawe wa kiume. Tuliona o—ono la mti ukivunjwa mahali fulani, naye mtu huyo akaanguka, nusura kuvunjika mgongo wake.

Akampeleka hospitalini. Na usiku huo Bwana alinifunulia, kwangu, huo ulikuwa ndio mwisho wa sigara.

Kwa hiyo kesho yake alitaka sigara. Nikasema, "Nitamnunulia ktoni na kumpelekea. Angalia tu uone, siku zake za sigara zimekwisha." Yeye hajawahi kuvuta moja tangu wakati huo, na hajataka moja tangu wakati huo. Mungu! Mungu!

Mnaona, jambo la kwanza unalopaswa kufanya ni kuja kwenye Chemchemi hiyo. Huna budi kuja kwenye Maji hayo, tambua si kitu unachoweza kufanya. Ni yale Yeye aliyokufanyia. Haikubidi kuchimba; haikubidi kuvuta; haikubidi kuacha hili; haikubidi kuacha kile. Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kufika kule na kunywa. Hivyo tu. Kama una kiu; kunywa!

55 Sasa, Yeye alikuwa Mwamba. Mungu alimpiga kwa ajili yetu, Naye akatoa wingi wa maji halisi, masafi. Angali anayatoa, leo, kwa ye yote ambaye ataamini. Hii ni neema Yake, bila shaka, kwa watu Wake, sisi.

Kuna kitu kama hicho pale, kama watu wa siku hizi, walio tayari kupokea kile wanachoweza kupata, bali hawataki kutoa huduma yoyote kwa malipo. Israeli walikuwa tayari ku—kunywa kutoka kwenye mwamba sasa, bali hawakutaka kumpa Mungu utumishi Wake uliomstahili.

Naye daima anatupa huduma. Mwajua, hata hatuwezi kupumua bila Yeye. Hatuwezi kupumua bila huduma ya Mungu. Hivyo ndivyo tunavyomtegemea Yeye. Na, hata hivyo, karibu ituvunje vipande viwili kama tukijaribu kufanya, itatubidi kumfanyia jambo fulani. Yeye anatuomba tufanye jambo fulani, twende tukamwone mtu fulani, twende tukamwombe mtu fulani, twende tukamsaidie mtu fulani, karibu lituvunje moyo, kufanya jambo hilo. Lakini hatutaki kumfanyia chochote kwa ajili ya huduma.

56 Malalamiko yake yalikuwa, "Wameniacha Mimi, Neno; nao wamekubali birika livujalo, badala yake. Wamekubali ... Wameniacha mimi, Niliye Chemchemi ya Uzima, Chemchemi ya Maji ya Uzima; nao wanatamani na wanaona afadhali kunywa kutoka kwenye birika lenye maji yaliyooza." Ungeweza kuwazia jambo hilo?

Ungeweza kuwazia mtu sasa, ambaye, hapa kuna kisima kinachofoka maji kinachotoa tu maji hayo mazuri, yatokayo kwenye mawe ya chokaa, moja kwa moja kutoka katikati ya miamba, huko chini kwenye matuta ya mchanga, na kadhalika, baridi tu na nzuri kama iwezavyo kuwa; na anaona afadhali anywe kutoka kwenye birika kule, ambayo yametitirika kutoka juu ya ghala, na mabanda, na majengo yote ya nje kuzunguka mahali hapo? Na kuyaweka kwenye birika hilo pale, ambapo maji yanayopenya huchuruzikia mle, kutoka kwenye ghala ya nafaka, na maboma na mazizi, na kila kitu kikichuruzikia kwenye hilo birika, halafu tunataka kuku-...tungenywea hilo kabla hatujaenda kwenye hicho kisima kinachofoka maji? Kutakuwa na kasoro fulani kiakili kwa mtu huyo. Hiyo ni kweli.

57 Na wakati mwanamume ama mwanamke atachukua msimamo wa madhehebu, yatakayoruhusu kukata nywele, kuvaa kaptura, vipodozi, kila namna ya hivi vitakataka vingine, na namna fulani ya m—mpango, na kufanya mambo haya yote yasiyofaa, na anaweza kwenda kwenye mchezo wa matufe, na—na upuzi huu wote kule, na anaweza kuvumilia mambo hayo; na kupenda hayo vizuri kuliko wanavyolipenda Neno la Mungu la mtindo wa kale ambalo hukata na kuchimba, na kuwafanya wanawake mabibi, na linawachukua na kuwafanya wavalie vizuri na kuenenda vizuri, linaondoa sigara na tumbaku, na kuapa na kulaani, na kudanganya na kuiba, mbali nawe, na ulimwengu wote kukutoka, na likakupa Kitu ambacho kinaridhisha kabisa. Kwa nini mwanamume ama mwanamke anaenda kwenye kitu kama hicho kwa ajili ya faraja? Unawezaje kupata faraja kutokana na jambo hilo?

58 Ungewezaje kupata maji mazuri kutoka kwenye birika lenye maji yaliyooza? Kwa nini mtu ... Kama mtu akienda kwenye birika la maji yaliyooza kupata maji ya kunywa, wakati tayari kuna kisima kinachofoka maji, ungesema, "Mtu yule ana kasoro bongoni."

Na kama mwanamke au mwanamume akienda mahali kama hapo kupata faraja, mtu huyo ana kasoro fulani kiroho. Hawataki Neno. Hawalitaki Neno. Inaonyesha ya kwamba asili yao ingali ya chura, ama kiluwiluwi, ama cho chote kile, hiyo ni kweli, kitu cha asili hiyo kinachopenda kidimbwi hicho chenye maji yaliyooza, kwa maana vitu vya aina hiyo havitaishi katika kidimbwi cha Maji masafi. Hawawezi kufanya hivyo; ni Maji masafi. Hawawezi kufanya hivyo.

59 Sasa, malalamiko yalikuwa, "Wameiacha." Na leo wamefanya jambo lile lile.

Sasa mwangalie yule mwanamke kisimani. Vema, yeye alikuja kwenye birika la Yakobo, naye alikuwa akichota maji pale wakati wote, kwenye birika la Yakobo. Lakini birika la Yakobo, dhehebu, tungeyaita, maana alichimba matatu; na hili alilochimba. Sasa, yeye alikuwa na hadithi kuu. Akasema, "Naam, baba yetu alichimba kisima hiki, Yakobo. Yeye alikunywa kutoka kwake, na ng'ombe wake wakanywa kutoka kwake, na kila kitu. Hiyo si ni nzuri vya kutosha?"

Yeye akasema, "Lakini maji unayochota humo, unaona kiu tena, inakubidi kurudi hapa na kuyateka tena. Lakini," kasema, "Maji nikupayo wewe ni Chemchemi, Chemchemi ya maji yanayoruka juu sana yakibubujika kutoka ndani, nawe hutakuja hapa kuyateka. Yamo pamoja nawe."

60 Angalia. Lakini alipoona kwamba Chemchemi ya Kimaandiko imemzungumzia, kwa ishara ya Kimaandiko ambayo alikuwa akiitazamia, aliiacha hiyo taratibu ya kimadhehebu ya Yakobo na hakurudi mle tena, kwa maana alikuwa ameupata ule Mwamba halisi. Mnaona? Alikimbilia mjini. Alikwisha acha dhambi. Hakuwa mwanamke mchafu tena. Alisema, "Njoni, mtazame Mtu niliyempata, Mtu aliyeniambia mambo niliyoyatenda. Je! Haiyumkini Huyu ndiye Kristo?" Yeye ... Hilo birika huenda lilikuwa ni sawa; lilikuwa limetimiza kusudi lake. Sasa yeye alikuwa kwenye ile Chemchemi ya kweli. Birika hilo lilikuwa sawa mpaka ile Chemchemi ya kweli ilipofunguliwa. Lakini wakati ile Chemchemi ya kweli ilipokuja, birika hilo lilipoteza nguvu zake. Aliona kuna mahali pazuri pa kunywa.

61 Na kuna mahali pazuri zaidi. Kuna mahali pazuri zaidi, na hapo ni katika Kristo. Katika Yohana Mtakatifu 7:37 na 38, Yesu alisema, mwishoni mwa sikukuu ya vibanda, "Mtu akiona kiu, na aje Kwangu, anywe."

Wote walikuwa wakifurahi. Wote walikuwa wakifurahi. Walikuwa na mbubujiko mdogo wa maji yakitoka chini ya madhabahu, na—nao wote walikuwa wakinywea huo, katika sherehe, ya—ya ile sikukuu. Ndipo akasema, "Baba zetu waliunywea mwamba wa roho jangwani." Mnaona, walikuwa wamejichimbia birika, maji yaliyooza waliyoyavuta kutoka mahali fulani, na kuyabubujisha mle chini ya hekalu pale. Nao wote wangezunguka kwenye maji haya na kunywa, na kusema, "Miaka mingi iliyopita, baba zetu walinywea jangwani."

Yesu alisema, "Mimi ndimi Mwamba ule uliokuwa jangwani."

Kasema, "Tulikula mana kutoka Mbinguni, na Mungu akainyesha."

Kasema, "Mimi ndiye Mana hiyo." Yeye, ile Chemchemi, alikuwa amesimama miongoni mwao. Huo Mkate wa Uzima ulikuwa umesimama miongoni mwao.

Na bado hawakuutaka. Afadhali wawe na birika lao; kwa sababu, mwanadamu alikuwa ametengeneza hii, na Mungu alikuwa amemtuma Ile. Hiyo ndiyo tofauti hasa. Walijichimbia mabirika!

Yeye alisema, "Mtu akiona kiu, na aje Kwangu, anywe." Yeye ndiye Chemchemi hiyo.

Na kama vile Maandiko yalivyosema, "Mito ya Maji yaliyo hai itatoka ndani yake." Loo, Yeye ndiye kisima hicho cha maji! "Kutoka ndani ya tumbo lake, au utu wa ndani kabisa, itatiririka mito ya Maji yaliyo hai."

62 Yeye ndiye ule Mwamba uliokuwa katika ... Huo ulikuwa Mwamba wa Hajiri, katika wakati wa shida; wakati mtoto wake mchanga alipokaribia kufa, wakati alipokuwa ameondolewa kambini, naye alikuwa huko nje pamoja na mtoto Ishmaeli. Maji yake, katika birika lake alilokuwa amebeba, yalikuwa yamekwisha. Naye akamlaza mtoto Ishmaeli chini; akaondoka akaenda, kadiri ya mtupo wa mshale, akalia, na, loo, kwa sababu hakutaka kumwona huyo mtoto akifa. Mara, Malaika wa Bwana akanena, naye akapata Beer-Sheba, kile—kile kisima kilichokuwa kinabubujika, na kingali kinabubujika hata leo. Alikuwa ni Beer-Sheba wa Hajiri, Mwamba huko nje nyikani.

63 Ilikuwa imesimama hapa katika Chemchemi iliyojaa Damu, siku hiyo, ikisimama pale hekaluni. [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] ... Wakati wa dhoruba. Katika Zekaria sura ya 13, Yeye alikuwa ile Chemchemi iliyofunguliwa katika nyumba ya Daudi, kwa ajili ya kusafisha, na kwa ajili ya (dhambi) kusafishwa kwa dhambi. Yeye alikuwa ndiye Chemchemi hiyo. Na katika Zaburi 36:9, Yeye alikuwa Chemchemi ya Uzima ya Daudi. Yeye angali ni Chemchemi hiyo katika nyumba ya Daudi.

Naye ni wa mshairi, moyoni mwake pale. Mshairi alisema:

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,  
Imetolewa kwenye vena za Imanueli,  
Wakati wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya mafuriko hayo,  
Hupoteza madoa yao yote ya hatia.

Yeye ndiye ile Chemchemi ya Uzima, Chemchemi ya Maji. Yeye ni Neno la Mungu.

64 Watu wa siku hizi za mwisho wamemwacha, Neno la kweli, Maji ya Uzima; na wamejichimbia mabirika ya kimadhehebu; na, tena, wakachimba, walichimba!

Na sasa tunaona, wamekuwa na mabirika yaliyovunjika. Na ndipo birika hili limejazwa na vijidudu visivyoamini, majivuno yasiyoamini, mipango ya elimu, na kadhalika, ambayo ni kinyume cha ahadi za Mungu. Wao ni wanaoshuku Neno.

65 Sasa, mabirika haya waliyo nayo, Biblia ilisema, yalikuwa "yanavuja." Birika lililovunjika ni birika "linalovuja," na linamwaga maji. Yanafanya nini? Yanaingia kwenye dimbwi la uchafu la kidini linaloitwa Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Na hapo ndipo birika linalovuja linapowaongoza, kwa sababu tu wamemwacha, na wame ... Chemchemi ya Maji ya uzima; na kujifanyia mabirika haya.

Wanachimba miradi mikubwa ya seminari ya masomo, elimu, na kadhalika. Hiyo ndiyo aina ya mabirika wanayochimba leo, ambapo mtu hana budi kuwa na Ph.D., ama LL.D., ama Shahada ya Sanaa, ama kitu fulani, kabla hata hajaenda kuhubiri. Mabirika ambayo yamejazwa na theolojia ya kujitengenezea. Wao wanawapeleka katika shule hizi kubwa mno za masomo, na humo wanawadunga kwa theolojia za kujitengenezea, na kuwatuma na hizo. Ni siku ya jinsi gani tunayoishi, mabirika ya kujitengenezea! Hakuna shida ... Si ajabu kitu hicho kimekuwa ni ki—uvundo, loo, jamani, ni kwa sababu watu wananywea humo.

66 Na wakati watu wanapotaka furaha leo, wanafanya nini? Watu, badala ya kuikubali furaha ya Bwana, wanageukia dhambi, kwa furaha. Watu wanaokwenda kanisani na kudai kuwa ni watumishi wa Kristo, wanapopata wasiwasi sana watawasha sigara. Na wakati wao—wakati wao wanataka ku—kujifurahisha, wanavaa nguo zao chafu na kutoka nje wakakate nyasi wakati wanaume wanapita, kusudi wawafanye wawapigie mruzi. Wanafanya kila kitu wapate kupendwa na watu. Wanataka kuonekana kama nyota wa sinema. Hiyo ndiyo furaha yao.

Wakati, Yesu alisema, “Mimi ndimi utoshelevu wao.”

Sababu ya wao kwenda kwenye jambo hilo, ni kwa sababu hawataki kunywa kutoka kwenye Chemchemi hiyo. Wameikataa. Hawataki kuinywa. Wamejiunga na namna fulani ya taratibu za kujitengenezea, namna fulani ya birika iliyojaa namna zote za vitu vilivyooza, waweze kwenda hivyo.

67 Jana, tulikuwa na watoto kule mtoni. Ninaamini ilikuwa Jumamosi asubuhi. Tulishuka kwenda; Billy alikuwa akivua samaki kwenye boti. Nasi tukawapeleka watoto, mjukuu wangu mdogo na hao wengine, binti yangu, na mwanangu mdogo, nasi tukaenda mtoni ku—kupanda boti. Usingeweza hata kupanda boti mtoni, kwa ajili ya watu wachafu, wachafu, watu waovu huko nje mtoni, wakiwa nusu uchi na wakiendelea. Boti ilienda kando yetu, kundi la wavulana wadogo wenye umri wa miaka kumi na miwili, kumi na minne, kila mmoja akiwa na kopo la bia mkononi mwake, na sigara. Wanaita jambo hilo “kufurahi.” Loo, jamani! Ulimwengu huu unaweza kudumu kwa muda gani, ukiwa na mfumo kama huo?

68 Kisha ili kujiepusha na mawazo kwamba watakapokufa wataenda kuzimu, jambo wanalofanya, wanaondoka wanaenda na kujiunga na mabirika haya ya kujitengenezea. Kwa hiyo watu wa aina hiyo ni wa birika hilo. Si kitu ila kundi la vifurukuta-mikia vichafu, na vyenye vinyaa vya ulimwengu. Nao wanajihusisha na jambo hilo kwa sababu, kama vile mama yangu mzee alivyokuwa akisema, “Ndege wa manyoya wanakusanyika pamoja.” Hawatakuja kwenye Chemchemi na kusafishwa kutoka kwenye maisha hayo ya dhambi. Wanataka kuishi huko nje, na bado wanashikilia ushuhuda ya kwamba wao ni Wakristo. Kwa nini? Wamemwacha, Chemchemi ya kweli ya furaha, Uzima, Maisha makamilifu na ya kuridhisha. Hiyo ndiyo sababu walifanya jambo hilo, kwa sababu wanataka kujiunga. Wana aina fulani ya watu pale wanaoamini upuuzi huo.

69 Hapa si muda mrefu uliopita, mimi na Ndugu Fred, na Ndugu Tom, baadhi yetu tulikwenda kuhudhuria kanisa maarufu la Kibatisti katika mji wa Tucson, kuona kama tusingepata kitu fulani kidogo ambacho labda kingetuburudisha kidogo. Naye mhudumu akasema jambo lingine kuhusu watu kule Misri, wakati walipoondoka walikuwa wakila vitunguu saumu na kadhalika, walitaka kurudi tena na kula hiyo. Kasema, “Hivyo ni kama walivyo watu siku hizi.”

Na, sisi, kila mtu alisema, “Amina!” Sijapata kuona kundi kama hilo! Kanisa zima likaacha kumwalia mhubiri likiangalia nyuma kuona ni nani aliyesema “amina.” Liliwaogopesha nusura wafe. Hawakujua ilikuwa ni kitu gani.

Wakati, Daudi alisema, “Mpigieni Bwana kelele za shangwe. Msifuni kwa vinubi! Msifuni kwa kinanda! Hebu kila kitu kilicho na pumzi na kimsifu Bwana. Na msifuni Bwana!” Mungu hufurahia watu Wake. Hebu na wale waliofunzwa, waseme, “Amina,” wakati lo lote limesemwa sawa.

70 Mbona usiache utaratibu huu na mabirika ya ulimwengu, uingie kwenye utaratibu mwaminifu wa Mungu, ambao ni kisima kinachofoka maji, Yesu Kristo? Mbona usimgeukie, ambapo Mungu ndiye atupaye wingi wa furaha yetu, ndiye atupaye wingi wa sifa, ndiye atupaye wingi wa kuridhika kwetu. Utulivu wa neva zangu hutoka kwa Mungu.

Wakati nimehuzunika sana, napata kuridhika kwangu katika Kristo, si katika sigara, si katika mambo ya ulimwengu, si katika kujiunga na baadhi ya kanuni za imani, lakini katika kumpata Yeye, Neno lililoahidiwa ambalo Yeye alisema, “Kama nikienda, nitakuja tena na kuwapokea.” Ninaona furaha yangu katika jambo hilo. Yeye ndiye Furaha yangu.

71 Wanasema leo, kwa kujiunga na mambo haya na kwa kuliunda Baraza hili la Makanisa Ulimwenguni, ya kwamba watafanya mahali pazuri pa kuishi. Kwa maoni yangu ya kweli, watafanya mahali pazuri pa kutenda dhambi. Hiyo ni ninii tu ... Kitu hicho chote ni dhambi, hata hivyo; si kuishi ndani yake, bali kufa ndani yake. Fanya mahali pake pa kutenda dhambi katika—dhambi ndani, badala ya kuishi ndani.

Kitu kingine chochote, nje ya Yesu Kristo na Neno Lake la Uzima, ni birika linalovuja. Kila

kinachojaribu kuwa badala Yake; kila unachojaribu kufanya kukuletea amani, kila unachojaribu kufanya kukupa faraja, kila namna ya furaha unayopata kutoka kitu kingine cho chote, kama kibadilisho cha Huyu, ni birika linalovuja lililojaa vinyaa. Yeye hutoa kuridhika kikamilifu.

72 Ninakumbuka hapa, majira kadhaa ya kiangazi yaliyopita, nilitoka kwenye mlango wa nyuma. Kulikuweco na kijana mlaghai mamboleo kule nje aliyeniambia, kasema, "Wajua, sababu ya wewe kuzungumza juu ya wanawake namna hiyo, kuvaa hizo kaptura na kadhalika," akasema, "ni kwamba wewe ni mzee." Kasema, "Hiyo ndiyo sababu."

Nikasema, "Angalia hapa. Una umri gani?"

Kasema, "Ishirini na saba."

Nikasema, "Nilipokuwa mdogo kwako kwa miaka mingi, nilihubiri jambo lile lile."

Nilipata Chemchemi ya kuridhika. Yeye ndiye fungu langu. Amina! Mradi tu Yeye anatoa hayo, huo ndio uzuri. Hiyo ni—hiyo ni ninii yangu ... Hiyo ni sanaa yangu, ni kumwagalia Yeye, kuangalia mkono Wake ukifanya kazi na kuona kile anachofanya. Hakuna chemchemi nyingine ninayojua!

Loo, mtiririko huo ni wa thamani  
Hilo linanifanya kuwa mweupe kama theluji;  
Sijui chemchemi nyingine,  
Hakuna kitu ila Damu ya Yesu.  
Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,  
Iliyotoka kwenye mishipa ya Imanueli,  
Ambapo wenye dhambi wakitumbukizwa ndani ya mafuriko hayo,  
Hupoteza mawaa yao yote ya hatia.

73 Ninawaambia, sijui chemchemi nyingine ila hiyo Chemchemi. Ilinisafisha nilipokuwa mchafu. Inaniweka msafi, kwa sababu nataka kuishi Mle, nipate kunywa haya Maji matamu yanayojaza nafsi yangu furaha.

Hata naweza nikawa nimeshushwa moyo sana, na kujisikia kwamba ni vigumu kwangu kuendelea, zamu nyingine, siwezi kwenda mahali pengine; ndipo naweza kupiga magoti na kuweka kidole changu kwenye ahadi, na kusema, "Bwana Mungu, Wewe Ndiye nguvu zangu. Wewe Ndiye uniridhishaye. Wewe Ndiye uniridhishaye. Wewe Ndiwe yote katika yote kwangu." Ninaweza kuanza kusikia kitu Fulani kikibubujika kutoka ndani yangu pale. Nilitoka kwake.

74 Kwa kuwa nishapita umri wa miaka hamsini, ninaamka asubuhi, mnajua jinsi ilivyo, ni vigumu kwako kuutoa huo mguu mmoja kitandani. Jamani, ni vigumu kufanya hivyo; na mtu fulani mlangoni, akibisha, ama Billy akiniambia kuna dharura, mahali fulani sina budi kwenda. Nami nafikiri, "Ninawezaje kufanya jambo hilo?" Jaribu kuweka mguu mmoja nje.

Nawazia, "Wewe ni Chemchemi iliyojaa nguvu zangu. Amina! Nguvu zangu na msaada wangu hutoka kwa Bwana. Wewe ndiye kisima changu kinachofoka maji! Wewe ndiwe ujana wangu! 'Hao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa kama tai; watapiga mbio, wala hawatachoka; watakwenda kwa miguu, wala hawatazimia.' Bwana Mungu, huu ni wajibu wangu, kwenda. Nimeitwa kazini." Na muda si muda, Kitu fulani kinaanza kuchemka ndani yangu.

75 Juzijuzi, huko kwenye sehemu ndogo, nilikuwa na mkutano hapa Topeka, Kansas; kulikuwako na mvulana, mhubiri kijana, mmoja wa wadhamini wangu wa kwanza. Ndugu Roy, anayeketi hapa, anakumbuka mahali hapo. Katika hili, katika mahali hapa pazuri pale, kulikuwako na—na ... Huyu mhudumu alikuwa ameingia chini ya paa ama mahali fulani, ukuta wa pembeni ukamponda chini ya huo. Maskini jamaa huyo alikuwa anakufa. Ini lake lilikuwa limepasuka. Wengu lake liliondolewa mahali pake. Tani kadhaa zilimwangukia.

Niliketi kwenye kiamshakinywa, nikizungumza na mke wangu. Nikasema, "Mke wangu, unajua, kama Yesu alikuwa hapa, unajua kile angefanya?" Nikasema, "Wakati aliponidhamini, 'Ninaamini hilo Neno,' alikuwa akimdhamini Kristo." Nami nikasema, "Huo ni ujanja wa ibilisi." Nikasema, "Kama Yesu angalikuwa hapa, angeenda kuweka mikono Yake mitakatifu juu yake. Mvulana huyo angepona. Sijali kama ini lake limepasuka. Angepona, kwa sababu Yesu angeingia mle ndani akijua Yeye alikuwa ni nani hasa. Yeye alijua wito Wake, Maandiko yalikuwa sahihi, yakithibitisha ndani Yake ya kwamba alijua Yeye alikuwa ni Nani, wala si ... bila shaka yo yote. Yeye angeweka mikono Yake juu yake, na kusema, 'Mwanangu, uwe mzima,' atoke pale." Nami nikasema, "Hakuna pepo wa kutosha kuzimu kumwua mvulana huyo, basi." Nikasema, "Yeye atapona." Lakini nilisema, "Unaona, mpenzi, Yeye alikuwa ni Yesu, mikono mitakatifu ya Mungu."

Nikasema, "Mimi ni mwenye dhambi. Nilizaliwa kwa kujuana kimwili. Baba yangu na mama yangu wote wawili walikuwa wenye dhambi, nami si kitu kabisa."

Nami nikasema, "Lakini unajua nini? Kama Bwana angenipa ono na kunituma kule, basi hilo lingekuwa

ni tofauti." Nikasema, "Ningeenda chini na kuweka mikono yangu juu yake, angetoka kwenye kitanda hicho kama Yeye akinipa ono."

76 Ndipo nikaanza kuwazia, "Hata hivyo, kama lilikuwa lile ono, lilikuwa ni nini? Ilikuwa ni mikono ile ile michafu juu yake, a-ha, mtu yule yule akimwombea, mikono michafu ile ile."

Ndipo nikaanza kuwazia, "Mimi ni mwakilishi Wake. Halafu, Mungu hanioni. Hiyo Damu ya yule Mwenye haki iko juu ya madhabahu; Hufanya upatanishokwa ajili yangu. Yeye ndiye utoshelevu wangu. Yeye ndiye ombi langu. Yeye ni Uzima wangu." Nikasema, "Kitu pekee ambacho kingenifanya niweke mikono yangu juu yake, kwa imani, kwa sababu nilikuwa na imani katika lile ono. Na bila ya ono, imani ile ile ingefanya jambo lile lile; kwa hiyo najihesabu mimi si kitu, bali namhesabu Yeye kuwa yote katika yote kwangu. Yeye ni Uzima wangu. Yeye Ndiye aliye niagiza. Hakuna dhehebu lililonituma; Yeye alinituma. Haleluya! Ninaenda katika Jina Lake. Nitamwekea mikono." Nikashuka kwenda kule na kumwekea mikono mvulana huyo, na usiku huo alikuwa mkutanoni, mzima kabisa. Amina!

77 Loo, naam, Yeye ndiye Chemchemi hiyo. "Hakuna kisima kingine ninachojua. Si kitu ila Damu ya Yesu!" Mimi ninanuka, mimi ni laghai, kila mmoja wetu ndivyo alivyo, bali mbele za Mungu sisi ni wakamilifu. Ye- ... "Kwa hiyo iweni wakamilifu, kama Baba yenu wa Mbinguni alivyo mkamilifu." Unawezaje kuwa? Kwa sababu aliye Mkamilifu hutuwakilisha pale. Hiyo Chemchemi ipo kila siku, safi. Si kitu fulani kilichooza, bali safi kila siku, ambayo husafisha dhambi zangu zote. Yeye ndiye Chemchemi hiyo.

78 Sasa katika kufunga, huenda nikasema jambo hili. Kila kilicho tofauti na Hiki ni mabirika yavujayo, na hatimaye yatamwaga yale utakayotia ndani yake; kama unaweka matumaini yako yote, wakati wako wote, na kila kitu, katika moja ya hayo mabirika yaliyooza. Yesu alisema ya kwamba yalikuwa mabirika yavujayo. Mungu alisema, "Yanavuja, yatamwaga cho chote unachotia ndani mwao." Huwezi kuendelea mbele zaidi nayo, kwa maana yatamwaga cho chote unachotia ndani. Kwa maana Yeye ndiye njia pekee ya kuelekea kwenye ile Kweli, kwenye Uzima, hata furaha ya Milele, na amani ya Milele. Yeye ndiye tu peke Yake na njia pekee ya kwenda Kule. Loo, jamani!

Chemchemi isiyoisha ya Uzima ni Yesu Kristo. Kwa nini? Na Yeye ni nani? Neno, lile lile; Neno, Uzima, Chemchemi, "yeye yule jana, leo, na hata milele." Mwamini wa kweli, ni furaha yake kuu, Uzima wake mkuu. Na kuridhika kwake ku kuu ni katika Kristo. Hakuna kusukuma, hakuna kuvuta, hakuna kujiunga, hakuna dhamana; kuamini tu na kupumzika. Hivyo ndivyo alivyo kwa waaminio.

79 Kama vile baba Ibrahimu; yeye hakuvuta kamwe, hakuhangaika, hakufadhaika. Yeye alikuwa na Neno. Alilala juu ya matiti ya El Shaddai. Wakati Ibrahimu alipokuwa na umri wa miaka mia moja, Mungu alimtokea, na kusema, "Mimi ni Mwenyezi." Neno la Kiebrania ni El Shaddai, linamaanisha, "Mwenye Matiti." "Nawe u mzee, na nguvu zako zimekwisha, lakini kaa kifuani Mwangu unyonye nguvu zako toka kwenye Chemchemi hii." Amina! Alinyonya hata akapata nini? Mwili mpya. Alipata mtoto, kwa Sara. Na, miaka hamsini baadaye, akapata watoto saba kwa mwanamke mwingine.

Loo, El Shaddai! Agano la Kale linaonyesha yale aliyofanya, Agano Jipya linaelezea yale atakayofanya. Amina! Katika Agano la Kale ...

80 Sasa hewa haibaridishwi, kwa hiyo nitaharakisha na kuondoka hapa sasa, katika dakika moja tu.

Ningetaka kusema jambo hili kabla sijafunga. Nilikuwa na mfano mzuri wa jambo hili wakati mmoja. Nilikuwa nikifanya doria. Na watu wengi hapa ... Huko chini karibu na Georgetown, huko chini Milltown, kulikuwa na, huko nyuma kabisa milimani, chemchemi. Ilikuwa ni kisima kinachofoka maji. Kingeyarusha nje, mkondo wa maji wa yapata fu—futi nne ama tano, yalichuruzika wakati wote, na pakawa na chemchemi kubwa mno pale. Na kila mahali kuizunguka kulikuwa na mirenaha hii hapa mingi, mwajua, vitu hivi vinavyokua hapa, kama mnanaa. Na, loo, nilikuwa na kiu tu ya kufika kule, loo, jamani, kufika kwenye chemchemi hiyo. Nami ningalilala karibu na kitu hiki na kunywa tu na kunywa, na kuketi chini na kunywa, kungojea.

Na mwaka baada ya mwaka bado ningekuja kwenye chemchemi hii hii. Haikukoma kamwe, majira ya kipupwe wala ya kiangazi. Hawangeweza kukigandisha. Huwezi kukigandisha kisima kinachofoka maji. Loo, la! Loo, la! Sijali jinsi—jinsi inavyokuwa baridi, haitakiganda hicho. Utagandisha birika; barafu kidogo tu itafanya hivyo. Mnaona?

Bali kila kinachosogea, kilicho na Uhai ndani yake, kinasogea huku na huko. Wala huwezi kugandisha Kisima kinachofoka maji. Hata roho iliyo mahali pale iwe ni ya huzuni namna gani, Kisima hiki daima ni hai. Ishi kwenye Kisima hicho.

81 Nami nikaona pale, nikapitia pale na ningekunywa, na, loo, jamani, maji safi tu! Haikubidi kamwe kuwa na wasiwasi, "Sijui, kama nikifika pale, sijui kama kimekoma kufoka tena?" Kimekuwa kikiendelea kufoka ...

Mkulima mzee aliniambia, kasema, "Babu yangu anakunywa kutoka kwenye hicho." Kisha akasema, "Hakijapungua kamwe wala cho chote kile. Bado ni kisima kile kile, kinachotiririka moja kwa moja mpaka

Blue River kule.”

Nikawaza, “Loo, jamani, ni mahali pazuri jinsi gani pa kumwagilia maji!” Ningetembea umbali wa maili moja kutoka njiani, kufika mahali hapo, kwa sababu ilikuwa mahali halisi pa kunywa. Loo, ni mazuri iliyoje hayo maji! Loo, jamani!

Ninge—ningeenda huko nje kwenye jangwa hilo, Arizona sasa, ningali ninawazia juu yake, “Kisima kile cha ajabu kule chini, laiti ningejilaza chini kule!”

Kama alivyosema Daudi wakati mmoja, “Loo, laiti ningalinywea kile kisima mara moja tena!” Laiti angefika tu kule!

82 Nami nikaketi chini siku moja, nami nilikuwa na jambo dogo la kuchekesha lililonipata. Nami nikasema, “Ni kitu gani kinachokufanya uwe na furaha sana wakati wote? Laiti ningaliweza kuwa na furaha namna hiyo. Mbona, sijapata kukuona ukiwa na huzuni, tangu nimekuwa nikija hapa. Hakuna hata jambo moja la huzuni kwako.” Nikasema, “Wewe daima umejaa furaha. Unarukaruka na kububujika na kuendelea. Kipupwe au kiangazi, baridi au joto, cho chote kile, daima umejaa furaha. Ni kitu gani kinachokufanya ...? Nini, ni kitu gani? Kwa sababu ninakunywa kutoka kwenu?”

“La.”

Ninasema, “Vema, labda sungura wanakunywa kutoka kwako, nawe unapenda sana.”

“La.”

Nikasema, “Vema, ni kitu gani kinachokufanya ububujike namna hiyo? Ni nini kinachokufanya uwe na furaha sana? Ni kitu gani kinachokufanya sikuzote kujaa furaha?” Kasema, “Je! Ni kwa sababu—kwamba ndege wanakunywa kutoka kwako?”

“La.”

“Kwa sababu nakunywa kutoka kwako?”

“La.”

Nikasema, “Vema, ni kitu gani kinachokufanya kujaa furaha sana?”

Na kama kisima hicho kingeweza kunijibu, kingesema hivi. “Ndugu Branham, si kwa sababu unakunywa; Ninathamini jambo hilo, na kwa sababu ninaweza kuwaandalia ndege. Mimi humpa mtu yeyote anayetaka kunywa. Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuja hapa na kunywa. Lakini, kinachonifanya niwe na furaha, si mimi kububujika, ni kitu fulani ndani, kinachonisukuma. Ni kitu kinachonibubujisha.”

Na hivyo ndivyo ilivyo na maisha yaliyojazwa na Roho. Kama vile Yesu alivyosema, Yeye alikuwa katika ... Unaona, Yeye anakupa visima vya maji yanayobubujikia Uzima wa Milele, kisima kinachofoka maji, maji yanayochuruzika ambayo daima yanatiririka. Kama kanisa lingine liko juu ama chini, ungali uko kwenye Kisima hicho.

Kwa nini uchukue taratibu ya kale ya kimadhehebu na birika, vilivyojawa na vimelea na kila kitu kinginecho, na kunywea kitu hicho chenye maji yaliyooza, ambapo huku umealikwa kwenye Chemchemi, Kisima kinachofoka maji?

83 Nafikiria jinsi kilivyosukuma tu, na kurusharusha, na—na kuchemka, na kucheka, na kufurahi, na kuruka, na kucheza. Kwenye baridi, mvua; joto, kukavu, wakati kwingine kote nchini kulikuwa kunashikwa na ukame, kilikuwa kikibubujika kama kilivyofanya daima. Kwa sababu kilikuwa kirefu, kikiwa na shina, kilitoka chini kabisa kwenye miamba.

Loo, hebu niishi karibu na Chemchemi hiyo! Chukua taratibu zako zote za kujitengenezea unazotaka, visima vyako vyote vya kale vya maji yanayooza, lakini hebu mimi nije kwenye...ama mabirika yenye maji yaliyooza. Lakini, hebu nije kwenye Chemchemi hii, hebu nije pale ambapo Yeye amejaa tu. Yeye ndiye Furaha yangu. Yeye ndiye Nuru yangu. Yeye ni wangu—Yeye ni Nguvu zangu. Yeye ni Maji yangu. Yeye ni Uzima wangu. Yeye ni Mponya wangu. Yeye ni Mwokozi wangu. Yeye ni Mfalme wangu. Kila kitu ninachohitaji kinapatikana ndani Yake. Kwa nini nitake kwenda kwenye kitu kingine chochote?

84 Ndugu, dada, hutakuja kwenye Chemchemi hii usiku wa leo? Hivi hutafanya hivyo, kama hujawahi kuwa kule, si utaupokea usiku wa leo tunapoviinamisha vichwa vyetu?

Mabirika yavujayo, yanamwaga, yanapenyeza, ulimwengu ukipenya mle ndani, vinyaa kutoka kwenye maghala ya nafaka na vya kutoka nyakati zingine. Mbona isiwe ni Kisima hiki, ambacho upuzi huo hauwezi kukaa mle, Chemchemi hii kuu iliyojawa na Damu, iliyotoka katika mishipa ya Imanueli? Kwa nini usipokee jambo hilo usiku wa leo? Mungu na atusaidie usiku wa leo, katika nchi hii kavu, yenye kiu. Kama vile nabii



alivyosema, "Yeye ni Mwamba katika nchi iliyochoka." Yeye ndiye Chemchemi hiyo. Mbona msije Kwake usiku wa leo, mioyoni mwenu, tunapoomba?

85 Mpendwa Baba wa Mbinguni, hakuna Chemchemi nyingine, kama muziki unavyocheza, "Hakuna chemchemi nyingine ninayojua; si kitu ila Damu ya Yesu." Nilizaliwa kule, nimelelewa kule; Ninataka kuishi pale, na kufa pale, na kufufuka tena kule, katika Uwepo Wake. Daima, Bwana, hebu niwe katika Uwepo Wake, kwa kuwa hakuna mwingine ninayemjua. Hakuna kanuni za imani, hakuna upendo; hakuna upendo ila Kristo, hakuna kanuni ya imani ila Kristo, hakuna kitabu ila Biblia, hakuna kitu kingine chochote, hakuna furaha nje Yake. Kumtoa kwangu, Ee Mungu, sijali nimemiliki ulimwengu kiasi gani, i—ingekuwa mauti, ningezunguka kila mahali huku nimeweka mikono yangu juu ya kichwa changu. Kumtoa kwangu, ningega dunia, Bwana. Lakini hebu na awe ndani yangu, halafu Desemba ni ya kupendeza kama Mei, basi hakuna mahali pa moto wala hakuna mahali pakavu, hata mauti yenyewe hayana ushindi. Hebu na tumpate Yeye, Baba. Mtoe, kwa wingi, kwa kila mwamini hapa usiku wa leo, kwa kuwa wamengoja katika chumba hiki.

Wengi wao hawana budi kuendesha magari barabarani usiku wa leo, wanapoenda makwao, na jalia hili liwe ndilo wazo lao, "Ninaishi kwenye ile Chemchemi. "Mimi ninaishi kwenye ile Chemchemi. Ninaishi hapo, nikinywa maji upya, saa baada ya saa."

Na iwapo hawajaipokea hiyo, bado, jalia wampokee sasa, kusudi waondoke waende pamoja na ile Chemchemi. "Nitaenda pamoja nanyi; Nitakuwa pamoja nanyi hata ukamilifu wa dahari." Yajalie mambo haya, Baba.

86 Na sasa wakati tumeinamisha vichwa vyetu, je! Kuna mtu hapa ndani, usiku wa leo, ama ni wangapi wangesema, "Bwana, nipeleke kwenye ile Chemchemi sasa hivi. "Bwana, nipeleke kwenye chemchemi hiyo sasa hivi. Kamwe sikuja hapa kusikia tu; naja hapa kutafuta Kitu fulani. Nimekuja hapa kukupata, Bwana. Nina haja nawe usiku wa leo. Njoo moyoni mwangu sasa hivi. Utafanya hivyo, Bwana?" Mungu akubariki. Bwana ambariki kila mmoja.

87 Baba, uliiona mikono, hata juu na kuzunguka ukuta, na katika vyumba vingine, nje. Wewe—Wewe umeiona, Baba. Na—naomba ya kwamba utawapa kila kitu wanachohitaji. Labda wamekuwa wakinywea birika fulani la kale, Bwana, kituo fulani cha katikati ambapo mtu fulani alichimba birika, limekwisha kuambukizwa na namna zote za mafundisho ya kigeni, likikana Neno. Ninaomba, Mungu, ya kwamba usiku wa leo watamjia Yeye ambaye ndiye Chemchemi hiyo, Chemchemi hiyo ya Uzima. Tujalie, Baba. Ninawakabidhi Kwako sasa katika Jina la Yesu.

Nawe uliniambia, "Ukiomba lo lote katika Jina Langu, litatendeka." Sasa, nisingeomba jambo hili, Bwana, kama sikufikiria lingetendwa. Ninge—ningekuwa nikilisema kwa utaratibu wa dini. Lakini ninawaombea, kwa uaminifu. Ninawaombea, nikiamini ya kwamba utatujalia yale uliyohidi.

Na sasa ninawaondoa kwenye birika hilo usiku wa leo. Ninawaondoa mahali walipokuwa wakinywea, ambapo hawaridhiki; kwenye Chemchemi hii. Ninafanya hivyo katika Jina la Yesu Kristo.

Wao ni Wako, Bwana. Hebu na wanywe kutoka Kwako, Maji yaliyo hai, Chemchemi ya Maji yaliyo hai. Katika Jina la Yesu, ninaomba. Amina. Tujalie, Bwana.

Ee, ni bubujiko la thamani  
Lile linanifanya mimi mweupe kama theluji;  
Mimi sijui kijito kingine,  
Hakuna kingine ila Damu ya Yesu.  
Ni kitu gani kiwezacho kuosha dhambi yangu?  
Hakuna kingine ila Damu ya Yesu;  
Kitu gani kiwezacho kunifanya mzima tena?  
Hakuna kingine ila Damu ya Yesu.

Ee Yesu, waponye hawa, Bwana! Tujalie, Bwana, kupitia Jina la Yesu. Naomba, Mungu, kwamba Wewe ...?... Wewe unajua mambo yote.

Mimi sijui kijito kingine,  
Ee, hakuna kingine ila Damu ya ...

88 Wazia jambo hilo, sijui chemchemi nyingine! Sijui kitu kingine ila Yeye. Sitaki kujua kitu kingine ila Yeye. Hakuna kingine ila Damu ya Yesu! Loo!

Ee, ni bubujiko la thamani  
Lile lifanyalo mimi mweupe kama theluji;  
Mimi sijui kijito kingine,  
Ee, hakuna kingine ila Damu ya Yesu.

89 Tunapoimba huo tena, na tupeane mikono sisi kwa sisi. Je! Mnapendana? Kuna mtu ye yote hapa aliye na jambo lo lote dhidi ya mtu mwingine? Kama yupo, nenda kaliweke sawa. Utafanya hivyo? Hebu

tusiondoke hapa namna hiyo. Mnaona? Kama una jambo dhidi ya mtu ye yote, nenda kaliweke sawa, sasa hivi. Sasa hivi ni nafasi yako ya kwenda kule, useme, "Ndugu, dada, nilisema jambo fulani kukuhusu, nilifikiri jambo fulani. Sikumaanisha kufanya hivyo. Nisamehe." Mnaona, hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo. Hebu na tuwe na Chemchemi moja kwa moja miongoni mwetu, wakati wote. Mnaona?

Hakuna kingine ila Damu ya Yesu,  
Hakuna kingine ila Damu ya Yesu.  
Ee, ni bubujiko la thamani  
Lile linifanyalo mimi mweupe kama theluji;  
Loo, mimi sijui kijito kingine,  
Hakuna kingine ila Damu ya Yesu.

Loo, Yeye si ni wa ajabu? Hakuna bubujiko lingine! Hatutajichafua wenyewe kwa mambo mengine. Tumejitenga, tumeuacha ulimwengu nyuma. Hatutaki tena vitunguu saumu vya Misri na mabirika yaliyovunjika. Tuko safarini pamoja na Bwana Yesu, ule Mwamba uliopigwa, amina, tukila Mana kutoka Juu, na kunywa; tukila Chakula cha malaika, na tukinywa kutoka kwenye Mwamba. Amina!

Mimi sijui kijito kingine,  
Hakuna kingine ila Damu ya Yesu.

Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu.

90 Tukiomba ya kwamba Mungu atambariki sana kila mmoja wenu, ili kwamba neema Yake na rehema ziwe pamoja nanyi katika juma lijalo. Na kama lo lote likitukia, kwamba mmoja wenu apenye aende upande wa pili wa pazia sasa, kumbuka tu ni usingizi na raha ya masaa machache tu hata tutakapokutana. Kumbukeni, ya kwamba, "Hao walio hai na waliosalia hawatawatangulia hao waliokwisha kulala mauti, kwa maana Parapanda ya Mungu, ile Parapanda ya mwisho..." Ya sita tayari imepigwa. Na Parapanda hiyo ya mwisho, kama ile Muhuri ya mwisho, itakuwa Kuja kwa Bwana. "Italia, nao waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza." Ni kupumzika tu mpaka wakati huo.

Na kama ukijeruhiwa, kumbuka:

Peleka Jina la Yesu,  
Akiwa ngao kutoka kila mtego;  
Wakati majaribu yanapokukusanyikia,  
Upumue tu Jina hilo takatifu katika maombi. (Mashetani watakimbia.)

Kumbuka tu, tunatarajia kukutana nanyi hapa Jumapili ijayo asubuhi. Waleta wagonjwa na wanaoteseka. Nitakuwa nikiwaombea. Ninyi niombeeni sasa. Utafanya hivyo? Sema, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Nitawaombea, ya kwamba Mungu atabariki.

... Jina katika maombi.  
Jina la thamani, Jina la thamani, Ee ni tamu iliyoje!  
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;  
Jina la thamani, Ee ni tamu iliyoje!  
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.  
Kwa Jina la Yesu kuinama,  
Naanguka kifudifudi miguuni Pake,  
Mfalme wa wafalme Mbinguni tutamvika taji,  
Wakati safari yetu itakapokamilika.  
Jina la thamani, Jina la thamani, (si ni tamu na la thamani?)  
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;  
Jina la thamani, Jina la thamani, Ee ni tamu iliyoje!  
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

91 Daima ni vigumu sana kukuacha. Ingawa ninajua ya kwamba unaungua, lakini kuna kitu fulani tu kuhusu ... Hebu, kifungu kimoja zaidi cha kitu fulani, mtafanya hivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Utafanya hivyo? Kibarikiwe Kifungo Kinachofunga, dada. Ni wangapi wanaojua ule wimbo wa kale? Tulikuwa tukiimba, miaka mingi iliyopita.

Nami nilikuwa nikiwazia, usiku wa leo, "mikono miwili, kati ya mamia ya ambao wamekwisha kuaga dunia," tulipokuwa tukiimba huo wimbo kwenye Maskani, na kushikana mikono sisi kwa sisi. Kibarikiwe Kifungo Kinachofunga. Nimezika wengi wao, papa hapa makaburini. Wanangojea. Nitawaona tena. Ninawaona, mara kwa mara, katika ono, ninapoangalia ng'ambo ya pazia. Wako pale.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa tunapoimba.

Kibarikiwe kifungo kinachofunga  
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;  
Ushirika ...  
Ni kama ile ya Juu.  
Wakati sisi ...

Sasa nyosha mkono na ushike mkono wa mtu fulani.  
... Tunapotengana,

Sasa inamisha kichwa chako.  
Linatupa maumivu ya ndani;  
Lakini bado tutaunganishwa moyoni,  
Na kutumaini kukutana tena.

Huku vichwa vyetu vimeinamishwa. Ninamrudishia mchungaji ibada sasa, na aturuhusu tutawanyike katika ...



[www.messagehub.info](http://www.messagehub.info)

Mahubiri Na  
**William Marrion Branham**  
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7